# HOTUBA
## YA
# SIALKOT

na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian

Masihi Mau‘udi na Imam Mahdi[as]

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Tanzania

**HOTUBA YA SIALKOT**
Tafsiri ya Kiswahili ya: *Lecture Sialkot* (Urdu)

Imeelezwa na:
Hadhrat Mirza Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri: Sheikh Bakri Abedi Kaluta

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1904
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2014

© Islam International Publications Ltd.

Kimeenezwa na:
Islam International publications Ltd.
'Islamabad' Sheephatch Lane,
Tilford, Surrey GU10 2AQ, United Kingdom

Kwa Maelezo Zaidi:
**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744
**Kenya:**
Ahmadiyya Muslim Association
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +255222111031

Kimechapwa na:

ISBN:978-1-84880-539-2

# Maelezo ya Mwenezi

**Kuhusu Mwandishi**

Mwandishi wa kitabu hiki, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Mau‘udi na Imam Mahdias, alizaliwa tarehe 13 Februari 1835 huko Qadian, India. Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alijitolea kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo aliielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine alifanya kazi kubwa sana ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam pekee ndiyo dini illiyo sahihi na hai siku hizi inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua

kuwa Imam Mahdi na Masihi Mau‘udi, sawa na bishara za Kurani na Hadithi za Mtume[saw] na Biblia. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 197 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha mpango wa Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa aliye Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba].

**Kuhusu Kitabu**

Kitabu hiki ni hotuba ya Seyyidna Ahmad[as] iliyotolewa tarehe 2 Novemba 1904 mjini Sialkot mbele ya hadhara kubwa ya Waislam na Mabaniani. Kwa sababu hiyo kinaitwa “*Hotuba ya Sialkot*”.

Katika kitabu hiki kwa kulinganisha Islam na dini zingine amethibitisha ubora wa Islam. Ingawa mwanzoni dini zote zililetwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu lakini baada ya kudhihiri Islam Mwenyezi Mungu Aliacha ulinzi wa dini zingine na katika Islam wajadidi na wasuluhishi waliendelea kudhihiri.

Katika mlolongo huo Mwenyezi Mungu Amenituma katika karne kumi na nne ya Kiislam kujadidisha dini ya Islam.

Katika kitabu hiki Syyidna Ahmad[as] mara ya kwanza kabisa alidai kuwa Krishna kwa Mabaniani. Akaeleza kwamba Raja Krishna alikuwa mtu mkamilifu aliyekuwa mkubwa katika manabii wa Mabaniani na alikuwa Nabii wa zama zake na alishukiwa na Malaika. Akiwa Krishna, Seyyidna Ahmad[as] amesahihisha baadhi ya makosa ya Maariya.

Mwishoni ameeleza hoja chache za ukweli wa madai yake zilizotajwa ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi kwa kudhihiri kwa Masihi Mau'udi na ametaja funuo na bishara zake zilizotangazwa mbele ya dunia katika hali ngumu na sasa zimeshatimia tayari.

**Shukrani**

Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta. Halafu Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania na Kenya na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbasihiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania, wakaichunguza na

kusahihisha tafsiri hii na kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana.

Aidha ndugu kadha wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Sharifu Tanwir Mujtaba, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal na Mubarik Mehmud marehemu.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin. Tafsiri hii ni tunda la Deski ya Kiswahili.

Chaudhry Muhammad Ali M.A.
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid
Rabwah. Pakistan
01.05.2014

**(Picha ya jalada la kwanza)**

هُدًی لِّلْمُتَّقِیْن

رسید مژدہ ز غیبم کہ من ہماں مردم — کہ او مجدد ایں دین و رہنما باشد

منم مسیح بہ بانگ بلند میگویم — منم خلیفہ شاہے کہ بر سما باشد

چنیں زمانہ چنیں دور ایں چنیں برکات — تو بے نصیب شوی وہ چہ ایں شقا باشد

سیاہ باد رخ بخت من اگر بدلم — دگر غرض بجز از یار آشنا باشد

خدا کے مُرسل

# حضرت مسیح موعود مہدی معہود

## عالی جناب میرزا غلام احمد صاحب قادیانی

کا لیکچر موسومہ بہ

# اسلام

جو ۲ نومبر ۱۹۰۴ء کو بمقام سیالکوٹ ایک عظیم الشان جلسہ میں پڑھا گیا

جس کو

چوہدری مولا بخش صاحب بھٹی احمدی نائب محافظ دفتر ضلع سیالکوٹ نے

مفید عام پریس شہر سیالکوٹ میں چھپوا کر شائع کیا

جلد ۱۲۰۰ قیمت فی جلد ۲ر

**(Tafsiri ya picha ya jalada la kwanza)**

Mwongozo kwa wamchao

*Imenijia habari njema toka kwa ghaibu kwamba mimi ndimi yule mtu aliye Mujaddidi wa Mwongozi wa dini hii. Mimi ndimi Masihi, naisema kwa sauti ya juu, mimi ndimi Khalifa wa Yule Mfalme aliye mbinguni.*
*Wakati kwa huu zama kama hizi na baraka kama hizi! hata hiyo kama ukizikosa, basi ilioje bahati yako mbaya!!*
*Bahati yangu iwe mbaya sana kama moyoni mwangu mna shabaha yoyote minghairi ya Mungu.*

Hotuba ya Mjumbe wa Mungu

**Hadhrat Masihi Mau'udi na Mahdi wa zama[as]**

**Mheshimiwa Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian**

iitwayo

# Islam

iliyosomwa tarehe 2 Novemba 1904 AD mjini Sialkot katika hafla adhimu.

Iliyo chapwa na

Chaudhari Maula Bakhsh Ahmadi Bhatti Naibu mhifadhi wa ofisi ya wilaya Sialkot katika kiwanda cha Mufide Aam Sialkot

Nakala 1200 Bei 2 Anna

**(Maelezo ya Bwana Maula Bakhsh Ahmadi Bhatti wa Sialkot)**

*Ujaji wa Mahdi aliyeahidiwa ubarikiwe, ufikaji wa Masihi Mau'udi ubarikiwe.*

*Leo mji wa Sialkot umekuwa sababu ya wivu kwa Firdausi na pepo ibarikiwe kuzidisha heshima nzuri.*

*Leo Imam mkuu ameshafika duniani, mwamuzi mwadilifu na asifiwaye abarikiwe.*

*Ee Mola Mkarimu! Kupitia kwake utusamehe, fadhili, rehema na ukarimu wako ubarikiwe.*

Ardhi ya Sialkot Ameiteua Mwenyezi Mungu hivi kwamba humo wamekuwapo kwa wingi wanaohami Jumuiya hii tukufu ya Mungu wenye nyoyo zilizojaa ikhlasi na upendo. Hadhrat Masihi Mau'udias aliporudi kutoka safari ya Lahore, ndipo kwa kuombwa na Jumuiya ya Sialkot kwa kusisitizwa Hudhuras aliye hisani tupu na rehema akawasili Sialkot tarehe 27 Oktoba 1904 pamwe na ahli na masahaba zake kwa garimoshi akipitia Lahore. Njiani kwenye stesheni zote wanajumuiya wa Jumuiya za hapo wakahudhuria kwa shauku sana kumlaki. Jioni saa kumi na mbili na nusu akawasili stesheni ya Sialkot. Mashekh wapinzani tayari wakikasirika kwa waadhi wa Maulawii Abdul Karim walikuwa

wameshughulika kuwapoteza watu wa kawaida na walikuwa wakisema katika nyaadhi zao kwamba mtu atakayekwenda hata kumwona Mirza sahib ndoa yake itabatilika na atakuwa ameritadi. Lakini Mungu hafanikishi upinzani wao wa namna hii. Watu wenyewe wakapata jazba na wakawa na shauku ya kumwona kiasi hiki kwamba mapema maelfu ya watu wakajumuika kwenye stesheni, platfamu, barabarani na madukani na alipowasili Hudhur ikawa kama sherehe kubwa sana. Na kwa wiki nzima ikaonekana jazba na shani kubwa ya dini ambayo mfano wake mpaka leo haukuonekana.

Mpango iliofanya Jumuiya ya Sialkot kukirimu wageni ulikuwa mzuri sana na wa kupendeza kwa kila jiha. Kwa kweli hii ilikuwa nafasi yenye baraka sana kwa Jumuiya ya Sialkot kwamba kukaa baina yao Masihi Mau‘udi aliandika hotuba hii na ikasomwa. Enye wakaaji wa mji ambao aliyetumwa na Mungu anaupenda sawa sasa na pale alipozaliwa, mbarikiwe kwani Masihi wa Mungu akawajieni, nanyi mlipata heshima ya kufanya mkutano huu adhimu. Ee ardhi, ubarikiwe na ufurahi na uimbe nyimbo za furaha kwamba Mahdi akakujia.

Ee Masihi wa Mungu, ee Krishna mwuaji wa nguruwe, mtunzi wa ngombe! Usifiwe duniani, watu wapate nuru ya mwongozo kwa baraka ya miguu yako na watoke kutoka katika shimo la upotevu. *Amin*.

Ni mimi

**Maula Bakhsh Ahmadi Bhatti mkazi wa Chwinda, Tarafa Zafarwaal, wila ya Sialkot.**

Kwa sasa naibu mhifadhi wa ofisi y a wilaya Sialkot

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]

نَحْمَدُهٗ وَ نُصَلِّی عَلَی رَسُوْلِهِ الْکَرِیْمِ[2]

# ISLAM

Kama dini zilizopo duniani zikitazamwa, itafahamika kwamba, mbali na Islam, kila dini ina kosa la aina fulani ndani yake. Na hii sio sababu kwamba dini zote hizo kwa hakika zilikuwa za uongo tangu mwanzo; bali ni kwa sababu kwamba baada ya kudhihiri kwa Islam, Mungu Aliacha kuzisaidia dini hizo, nazo zikawa kama ile bustani isiyo na mlimaji, na ambayo hakukuwa na utaratibu wowote wa kuinyweshea maji wala kuisafisha, basi uharabifu ukazalika humo hatua kwa hatua. Miti yote yenye matunda ikakauka na mahali pake ikaenea miba na manyasi mabaya, na hali ya kiroho, ambayo ndio mzizi wa dini, ikatoweka kabisa na ikawa imebakia maneno tu matupu. Lakini Mungu Hakuifanyia hivyo Islam. Na kwa sababu Alikuwa Anataka bustani hii idumu kustawi, basi

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

katika kila karne Akainyweshelea upya bustani hii na kuiokoa isikauke. Ingawa kila alipoinuka mja wa Mungu kurekebisha mwanzoni mwa kila karne, basi majahili waliendelea kumpinga na wakachukia mno isije likarekebika kosa ambalo tayari lilishaingia ndani ya desturi na mila yao. Lakini Mwenyezi Mungu Hakuiacha suna Yake hata kwamba katika zama za mwisho ambapo kuna vita ya mwisho baina ya uongofu na upotofu, Mungu Akaikumbuka ahadi Yake tena Akiwakuta Waislamu katika mghafiliko mwanzoni mwa karne ya kumi na nne, na elfu ya mwisho, na Akaijadidisha dini ya Kiislamu. Lakini dini zingine, baada ya kudhihiri Mtume wetu[saw], kamwe hazikupata ujadidisho huu. Kwa hiyo dini zote hizo zikafa, ndani mwao hamkubakia tena ucha Mungu na makosa mengi yaligandamana ndani mwao kama vile nguo iliyogandamana na uchafu kwa kutumika sana ambayo isifuliwe kamwe. Na watu kama hao ambao hawakuwa na mwelekeo wowote wa kiroho na ambao nafsi zao ziamrishazo kufanya maovu zilikuwa hazikutakasika na uchafu wa maisha mabovu, sambamba na matashi ya nafsi zao wakiziingilia dini hizo bila sababu yoyote na wakazipotosha kiasi hiki kwamba sasa zimekuwa kitu

kingine kabisa. Kwa mfano, itazameni dini ya Kikristo namna ilivyokuwa imejikita mwanzoni kwenye msingi safi, na mafundisho aliyoyatoa Hadhrat Masih[as] ingawa yalikuwa na upungufu ukilinganisha na yale ya Kurani Tukufu — kwani ulikuwa haujafika bado wakati wa mafundisho makamilifu na vipawa dhaifu (vya watu wale) havikuwa pia na uwezo huo — hata hivyo mafundisho hayo, kulingana na hali za wakati huo, yalikuwa mafundisho bora kabisa. Hayo yakaongoza kwenye Mungu Yule Yule ambaye kwaye Taurati ikaongoza. Lakini baada ya Hadhrat Masih[as], Mungu wa Wakristo akawa mungu mwingine ambaye hakutajwa hata kidogo ndani ya mafundisho ya Taurati, wala wana wa Israeli hawana habari yake katu. Kwa kumwamini mungu huyu mpya taratibu yote ya Taurati ikapinduka, na ile miongozo ilyokuwemo ndani ya Taurati kwa kupata wokovu wa kweli na madhambi na kwa kupata utakaso, yote ikawa imevurugika kabisa na mategemeo yote ya kujitakasa na madhambi yakawa kukubali kuwa Yesu mwenyewe aliridhia kufa msalabani kwa kuiokoa dunia, naye mwenyewe alikuwa ni Mungu. Na siyo hiyo tu, bali maamrisho mengine mengi ya kudumu

ya Taurati yakavunjwa, na yakatokea mabadiliko ndani ya dini ya Kikristo kiasi ya kwamba hata kama Yesu mwenyewe aje tena, hataweza kuitambua dini hii. Ni jambo la kushangaza mno kwamba wale watu ambao walisisitizwa sana kufuata Taurati wao wakaachana mara moja na maagizo ya Taurati. Kwa mfano, hakuna agizo ndani ya Injili kwamba japo nguruwe imeharamishwa ndani ya Taurati lakini mimi nami nawahalalishieni, na kwamba ndani ya Taurati imesisitizwa sana kutahiri lakini nalitangua agizo la kutahiri. Sasa lini ilijuzu kwamba yale maneno ambayo hayakutoka kwenye kinywa cha Yesu yaingizwe ndani ya dini! Lakini kwa kuwa ilibidi Mungu Aistawishe duniani dini ya wanadamu wote, yaani Islam, hivyo kuharibika kwa Ukristo ilikuwa ni kama alama ya kudhihiri kwa Islam. Jambo hili pia limeshathibitika kuwa dini ya Kibaniani nayo ilikuwa imeshaharibika kabla ya kudhihiri kwa Islam na ibada ya masanamu ilikuwa imeshaenea kwa ujumla katika India yote. Na hizi ni alama zilizobakia za uharibifu huo kwamba Yule Mungu Ambaye Hahitaji maada katika kuzitumia sifa zake, sasa kwa maoni ya Waarya Amelazimika kuhitaji maada katika kuumba viumbe. Kutokana na itikadi hii mbovu

wakalazimika kuikubali itikadi nyingine mbovu iliyojaa ushirikina, nayo ni kwamba chembe zote za ulimwengu na roho zote ni za tangu kale na zipo zenyewe. Lakini inasikitisha kwamba kama wangezingatia sana sifa za Mungu, wasingeweza kusema hivyo hata kidogo, kwa sababu kama Mungu katika kutumia sifa ya uumbaji — ambayo Yeye Anayo tangu kale — Anahitaji maada kama anavyohitaji binadamu, basi kwa sababu gani katika sifa Yake ya kusikia na kuona na mengineyo asihitaji maada kama binadamu. Mwanadamu hawezi kusikia chochote bila kuwepo hewa wala hawezi kuona chochote bila kuwepo nuru. Je na Mungu pia Anao udhaifu huo ndani mwake? Naye pia anahitaji hewa na mwanga kwa ajili ya kusikia na kuona? Hivyo, kama Yeye Hahitaji hewa wala mwanga basi mfahamu kwa yakini kwamba hata katika sifa ile ya uumbaji Hahitaji maada yoyote ile. Mantiki hii ni ya uongo kabisa kwamba Mungu Anahitaji maada yoyote katika kuzidhihirisha sifa Zake. Kuzikisia sifa za mwanadamu kwa Mungu kwamba haiwezekani kuumba toka kwenye kutokuwepo hadi kwenye kuwepo na kuuambatanisha udhaifu wa mwanadamu kwa Mungu ni kosa kubwa. Dhati ya mwanadamu ina

kikomo na dhati ya Mungu haina kikomo. Hivyo, Yeye Huumba dhati nyingine kutokana na nguvu ya Dhati Yake. Na huu ndio Uungu. Yeye Hahitaji maada yoyote katika sifa Yake yoyote, ama sivyo siye Mungu. Je, kwaweza kuwepo kizuizi chochote ndani ya kazi Zake? Na kwa mfano kama Atake kuziumba mbingu na ardhi kwa mkupuo, je, Hawezi kuziumba? Miongoni mwa Wabaniani waliokuwa na sehemu fulani ya kiroho pia pamoja na elimu na hawakuwa wenye mantiki isiyo na maana, hawakuwa na itikadi hii hata kidogo ambayo Waarya wameitoa siku hizi juu ya Mungu. Haya ni matokeo ya kukosa kabisa hali ya kiroho.

Ilimuradi, uharibifu wote huo uliotokea ndani ya dini hizo, ambao baadhi yake haustahili hata kutajwa na ambao unapingana pia na utakaso wa mwanadamum, alama zote hizo zilikuwa ni za haja ya kuwepo kwa Islam. Mwenye akili analazimika kukiri kuwa muda fulani kabla ya Islam dini zote zilikuwa zimeshaharibika na zimeshakosa uhai wa kiroho. Hivyo Nabii wetu[saw] alikuwa ni Mujaddidi Mkuu kwa kuudhihirisha ukweli aliyeleta tena duniani ukweli uliokuwa umetoweka. Hakuna nabii yeyote aliyeshirikiana na nabii wetu[saw] katika fahari hii

kwamba yeye aliikuta dunia yote imo gizani na kwa kudhihiri kwake giza hilo likabadilika kuwa nuru. Taifa alimodhihiri yeye, taifa hilo zima likaachana na ushirikia na kushikamana na Tauhidi kabla hajafa yeye. Sio hiyo tu, bali watu hao walifikia madaraja ya juu ya imani, na kazi zile za ikhlasi, uaminifu na uyakinifu zikadhihirika kwao ambazo mfano wake haupatikani katika sehemu yoyote ya dunia. Mafanikio haya na mafanikio kiasi hicho hakuyapata nabii yeyete minghairi ya Nabii Mtukufu[saw]. Hii ndiyo dalili kubwa ya ukweli wa unabii wa Mtume[saw] kwamba yeye alitumwa na kuja katika zama zilizogubikwa na giza totoro, na kitabia zikataka aje msuluhishi wa shani ya juu kabisa. Na halafu aliiaga dunia katika wakati ambapo malaki ya watu walikuwa wakishaacha ushirikina na ibada ya masanamu wakashikamana na Tauhiid (umoja wa Mungu) na njia iliyonyoka. Na kwa hakika marekebisho haya kamili yalikuwa ni makhsus kwake tu kwamba aliwafundisha mwenendo wa kibinadamu watu wale waliokuwa na sera za kishenzi na silika za kinyama. Au kwa maneno mengine tuseme kwamba aliwafanya wanyama kuwa wanadamu, na halafu akawafanya wanadamu hao kuwa wanadamu walioelimika, na

halafu akawafanya watu hao walioelimika kuwa waja wa Mungu, na akawapulizia uhai wa kiroho na kuwaambatanisha na Mungu wa kweli. Wakachinjwa kama mbuzi katika njia ya Mungu, na wakakanyagwa miguuni kama siafu, lakini hawakuiacha imani, bali wakapiga hatua mbele katika kila msiba. Hivyo, bila shaka Nabii wetu[saw] alikuwa ni Adamu wa pili katika kuustawisha uhai wa kiroho. Bali Adam wa kweli alikuwa ni yeye ambaye kwaye na kwa njia yake na kwa sababu yake fadhila zote za kibinadamu zilifikia kwenye ukamilifu, na nguvu zote njema zikaanza kufanya kazi zake, na hakuna tawi lolote la asili ya mwanadamu lisilobarikiwa na matunda. Na *ukhatam* wa unabii haukutokea kwake kwa sababu tu ya umwisho kizama, bali kwa sababu hii pia kwamba sifa zote kamilifu za unabii zimeishia kwake. Na kwa kuwa yeye alikuwa mdhihirisho kamili wa sifa za Mungu, kwa hiyo sheria yake imebeba sifa zote za Ujalali na Ujamali, na majina yake mawili ya Muhammad[saw] na Ahmad[saw] ndiyo kwa sababu hii hii. Na katika unabii wake ulio kwa watu wote hakuna sehemu yoyote ya ubahili, bali huo tangu mwanzo ni kwa ajili ya dunia nzima. Na dalili nyingine ya uthibitisho wa unabii wake ni kwamba kutokana na

vitabu vya manabii wote na halikadhalika kutokana na Kurani Tukufu pia inafahamika kwamba Mungu, kuanzia Adam hadi mwisho, Aliuweka umri wa dunia kuwa miaka elfu saba, na Akaweka duru za miaka elfu moja moja kwa ajili ya uongofu na upotofu. Yaani duru moja ni ile ambamo mwongozo unashinda na duru nyingine ni ile ambamo upotofu hupata ushindi. Na kama vile nilivyobainisha, ndani ya vitabu vya Mwenyezi Mungu duru zote hizi mbili zimegawanyika katika miaka elfu elfu. Duru ya kwanza ilikuwa ni ya ushindi wa mwongozo, humo hamkuwa hata na alama ya ibada ya masanamu. Ilipomalizika hii miaka elfu moja hapo ndani ya duru ya pili ambayo ilikuwa ni ya miaka elfu moja, aina mbali mbali za ibada ya masanamu zikaanza duniani na ushirikina ukashamiri, na ibada ya masanamu ikachukua nafasi katika kila nchi. Halafu ndani ya duru ya tatu iliyokuwa ya miaka elfu moja, humo msingi wa Tauhiid (Umoja wa Mwenyezi Mungu) ukawekwa na kadiri Mungu Alivyotaka Tauhiid ikaenea duniani. Halafu ndani ya duru ya elfu ya nne upotofu ukadhihirika na ndani ya hii hii elfu ya nne wana wa Israeli wakaharibika mno, na dini ya Kikristo ikakauka wakati ule ule mbegu yake

ilipopandwa, kama kwamba kuzaliwa kwake na kufa kwake ilikuwa katika wakati ule ule mmoja. Halafu ikaja duru ya elfu ya tano ambayo ilikuwa ni duru ya mwongozo. Hii ni elfu ile ambamo Nabii wetu[saw] alitumwa, na Mwenyezi Mungu Akaistawisha tena Tauhidi duniani kwa mkono wa Mtume Mtukufu[saw]. Basi hii hii ndiyo dalili madhubuti kabisa juu ya kutoka kwake kwa Mwenyezi Mungu kwamba kudhihiri kwake kulitokea ndani ya elfu ile ambayo tangu azali iliwekwa kuwa ya mwongozo. Nami sisemi haya kwa nafsi yangu, bali haya yanafahamika kutoka kwenye vitabu vyote vya Mwenyezi Mungu. Na hata madai yangu ya kuwa Masihi Mau'udi pia yanathibitika kutokana na dalili hii hii, kwani sawa na mgawanyiko huu, elfu ya sita ni elfu ya upotofu, na elfu hiyo inaanza baada ya karne ya tatu ya Hijra na kuishia mwanzoni mwa karne ya kumi na nne. Mtume[saw] aliwaita watu wa elfu hii ya sita jina "Faij A'waj" (watu wapotovu). Na elfu ya saba ni ya mwongozo ambamo sisi tumo ndani yake. Na kwa kuwa hii ni elfu ya mwisho, basi ilibidi Imam wa zama za mwisho azaliwe mwanzoni mwake, na baada yake hakuna Imamu yeyote wala Masihi yeyote ila yule atakayekuwa kama kivuli chake, Kwani ndani ya

elfu hii umri wa dunia sasa umefikia mwisho wake — jambo ambalo manabii wote walitoa ushuhuda juu yake. Na Imamu huyu anayeitwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni Masihi Mau‘udi, ndiye mujaddidi wa karne na pia mujaddidi wa elfu ya mwisho. Katika jambo hili hata Wakristo na Mayahudi pia hawahitilafiani kuwa zama hizi ni za elfu ya saba tangu Adam. Na kutoka muda tangu Adam mpaka sasa Alionidhihirishia Mungu kutokana na thamani kwa jumla ya herufi za sura Al-‘Asr pia yathibitika kuwa zama ambamo tumo hivi sasa ni zama za elfu ya saba. Na manabii waliafikiana juu ya hili kwamba Masihi Mau‘udi atadhihiri mwanzoni mwa elfu ya saba, na atazaliwa mwishoni mwa elfu ya sita, kwa sababu yeye ni mwishoni mwa wote kama vile Adam alivyokuwa mwanzoni mwa wote. Na Adam alizaliwa katika siku ya sita mnamo saa za mwisho za Ijumaa. Na kwa kuwa siku ya Mungu ni sawa na miaka elfu moja ya duniani, kwa kufananisha huku Mungu Akamwumba Masihi Mau‘udi mwishoni mwa elfu ya sita, kana kwamba ndiyo saa ya mwisho ya siku (ya Mungu). Kwa kuwa mwanzo na mwisho hulingana kwa namna fulani, hivyo Mungu Akamwumba Masihi Mau‘udi namna alivyomwumba Adam; Adam

alizaliwa pacha na alizaliwa mnamo siku ya Ijumaa, vivyo hivyo mimi, niliye Masihi Mau‘udi, nikazaliwa pacha na nikazaliwa siku ya Ijumaa. Na kuzaliwa kwenyewe kulikuwa hivi kwamba kwanza alizaliwa binti halafu nyuma yake nikazaliwa mimi. Kuzaliwa hivi kunaashiria kwenye ukhatam wa uwalii. Ilmuradi, haya ni mafundisho mwafaka ya manabii wote kuwa Masihi Mau‘udi atakuja mwanzoni mwa elfu ya saba. Ndiyo sababu katika miaka iliyopita kelele nyingi ziliibuka baina ya Wakristo, na huko Amerika majarida mengi yalitolewa juu ya habari hii kwamba Masihi Mau‘udi alikuwa adhihiri katika zama hizi hizi, kwa sababu gani hakudhihiri? Baadhi yao wakatoa jibu hili katika hali ya simanzi kuwa sasa wakati umeshapita, lifahamuni kanisa kuwa mwakilishi wake. Ilmuradi, hii ni dalili juu ya ukweli wangu kuwa mimi nimedhihiri ndani ya elfu ile iliyowekwa na manabii. Na hata kama kusingekuwa na dalili nyingine, basi dalili hii hii moja ilikuwa wazi sana iliyotosha kwa ajili ya mtafuta haki, kwa sababu kama hiyo ikataliwe, vitabu vyote vya Mwenyezi Mungu vinabatilika. Wale ambao wanayo elimu ya vitabu vya Mungu na wanaovisoma kwa kuzingatia, kwa ajili yao hii ni dalili wazi kama vile mchana

wenye mwanga. Kwa kuikataa dalili hii, unabii wote unakatalika, na hesabu yote inavurugika na nidhamu ya mgawo wa Mungu inaparaganyika. Hii si sahihi kama wadhanivyo baadhi ya watu kuwa hakuna yeyote mwenye elimu ya Kiama, basi ikadiriweje miaka elfu saba toka Adam hadi mwishoni? Hao ndio watu ambao hawakuwahi kuvitafakari sawasawa vitabu vya Mwenyezi Mungu. Mimi sikuikadiria leo hesabu hii. Hii imekubaliwa tangu zamani na wahakiki wa watu wa Kitabu, hata wanazuoni wa Kiyahudi pia wakaikubali. Na hata kutoka ndani ya Kurani Tukufu yafahamika kwa uwazi kabisa kuwa umri wa wanadamu kuanzia Adam hadi mwishoni ni miaka elfu saba, na vivyo hivyo vitabu vyote vya awali pia vinasema haya haya kwa kuafikiana, na hayo hayo pia yanatoka kutoka katika aya hii:

اِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَاَلْفِ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّوْنَ ۝۴۸ [3]

Na manabii wote kwa uwazi kabisa wamekuwa wakitoa habari hii hii. Na kama ambavyo nimekwisha eleza sasa hivi, hata kutokana na thamani ya herufi za sura “Al-‘Asr” inafahamika kwa uwazi kabisa kuwa

[3] Kwa hakika siku moja kwa Mola wako ni kama miaka elfu mnayoihesabu. *Al-Hajj*, 22:48

Mtume[saw] alidhihiri mnamo elfu ya tano tokea Adam, na kutokana na hesabu hii zama hizi tulizomo ni elfu ya saba. Lile jambo ambalo Mungu Amenidhihirishia kwa Wahyi Wake siwezi kulikataa wala sioni sababu yoyote ya kukatalia neno waliloafikiana manabii watakatifu wa Mungu. Basi, kama uthibitisho kiasi hiki upo, na bila shaka sawa na Hadithi na Kurani Tukufu hizi ndio zama za mwisho, halafu shaka ipi imebakia ya kuwa hii ndiyo elfu ya mwisho? Na ujaji wa Masihi Mau'udi mwanzoni mwa elfu ya mwisho ni jambo la lazima. Na kauli hii kwamba hakuna aijuaye saa ya Kiama, hiyo haimaanishi kwamba kwa jiha yoyote haijulikani. Kama ni hivyo, basi alama za Kiama zilizoelezwa ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi sahihi nazo hazitakuwa zenye kukubalika, kwa sababu kwazo pia yapatikana elimu ya kukaribia kwa Kiama. Mwenyezi Mungu Aliandika ndani ya Kurani Tukufu kwamba katika zama za mwisho kutakuwa na mifereji mingi duniani, vitabu vitaenezwa kwa wingi — magazeti pia yamo humo — na ngamia hawatatumika (kusafiri). Nasi twaona kwamba mambo yote haya yametimia katika zama zetu. Na badala ya ngamia biashara imeanza kutumia treni. Basi, tumefahamu kuwa Kiama kimekaribia, na

muda umepita ambapo Mungu Mwenyewe Alitupasha habari ya kukaribia kwa Kiama ndani ya aya ya "اِقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ[4]" na aya zingine. Hivyo, sheria haimaanishi kwamba kutokea kwa Kiama kumefichika kwa kila jiha, bali manabii wote wamekuwa wakiziandika alama za zama za mwisho, na ndani ya Injili pia zimeandikwa. Basi muradi wake ni kwamba hakuna aijuaye saa ile makhsus. Mungu Anaweza kuongeza karne chache baada ya kupita miaka elfu moja kwa sababu tarakimu isiyokamilika haihesabiwi, kama vile siku za ujauzito baadhi ya wakati huwa zinazidi. Tazameni! Watoto wengi wanaozaliwa duniani mara nyingi huzaliwa ndani ya miezi tisa na siku kumi, lakini hata hivyo inasemwa kwamba hakuna yeyote aijuaye saa hiyo ambapo uchungu wa kuzaa utaanza. Halikadhalika ingawa miaka elfu moja imebakia kufikia mwisho wa dunia, lakini saa ile haifahamiki kitakapotokea Kiama. Kuzipoteza dalili zile ambazo Mungu Amezitoa kwa ajili ya uthibitisho wa uimamu na unabii ni kama vile kuipoteza imani yako. Ni dhahiri kwamba alama zote za kukaribia Kiama zimejumuika na mapinduzi

[4] Kiama imekaribia. *Al-Qamar*, 54:2

makubwa yanashuhudiwa katika zama, na alama zile Alizozieleza Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu kwa kukaribia Kiama, nyingi katika hizo zimeshadhihirika. Kama vile inavyodhihirika toka ndani ya Kurani Tukufu, katika zama za kukaribia Kiama mifereji mingi itatiririka na vitabu vitaenea kwa wingi, milima itapeperushwa kama mavumbi ikiishasagwa, ardhi itastawi sana kwa kilimo, na njia zitafunguka kwa ajili ya kukutana kwa watu na tafrani za kidini zitatokea sana baina ya watu, kaumu moja itaiangukia dini ya kaumu nyingine kwa kishindo kama wimbi ili kuwaangamiza kabisa. Katika siku hizo hizo parapanda la kimbingu litafanya kazi yake na kaumu zote zitakusanywa katika dini moja isipokuwa wenye tabia mbaya ambao hawastahiki mwito wa kimbingu. Habari hii iliyoandikwa ndani ya Kurani Tukufu ni ishara kwenye kudhihiri kwa Masihi Mau‘udi na kwa sababu hii hii ikaandikwa katika habari za Yajuja na Majuja. Na Yajuja na Majuja ni kaumu mbili zilizotajwa ndani ya vitabu vya awali. Na sababu ya kuitwa jina hili ni kwamba hao watatumia sana *ajij* yaani moto nao watapata sana ushindi duniani nao watamiliki kila palipo juu. Hapo katika zama hizo hizo utafanyika mpango mkubwa

wa mabadiliko toka mbinguni na siku za suluhu na amani zitadhihirika. Hali kadhalika imeandikwa ndani ya Kurani Tukufu kwamba katika siku hizo machimbo mengi na vitu vingi vilivyofichika vitatokeza ardhini. Na katika siku hizo jua na mwezi vitapatwa mbinguni na tauni itaenea sana ardhini, na ngamia wataachwa, yaani utatokea usafiri mwingine utakaosababisha ngamia wasitumike. Kama tuonavyo kwamba shughuli zote za biashara ambazo hapo kabla zilikuwa zikifanywa kwa ngamia, sasa zafanywa kwa njia ya treni, na wakati unakaribia kwamba hata wale waendao kuhiji watasafiri kwa treni kuelekea Madina na siku hiyo Hadithi hii itatimia ambamo imeandikwa kwamba:

وليتركن القلاص فلا يسعٰى عليها[5]

Basi kwa kuwa alama hizi ni kwa ajili ya siku za mwisho ambazo zimeshadhihirika kikamilifu, basi kutokana na hiyo inathibitika kwamba miongoni mwa duru za dunia, hii ni duru ya mwisho. Na kama vile Mungu Alivyoziumba siku saba, na kila siku moja Ameifananisha na miaka elfu moja, basi kutokana na

[5] Na ngamia wanaachwa na hawatatumikia.

mshabihiano huu, umri wa dunia kuwa miaka elfu saba umethibitika kwa aya ya Kurani. Tena Mungu ni witri na huipenda witri, na kama vile Alivyoziumba siku saba kuwa witri na vivyo hivyo elfu saba pia ni witri. Kutokana na sababu zote hizo inaweza ikafahamika kuwa hizi ndizo zama ya mwisho na ndiyo duru ya mwisho ya dunia ambapo kudhihiri kwa Masihi Mau'udi mwanzoni mwake kumethibitika kutoka ndani ya vitabu vitakatifu. Na Nawab Siddik Hasan Khan anatoa ushahidi ndani ya kitabu chake 'Hujajul Karamah' kwamba mawalii wote wenye kuona kashfi waliopita ndani ya Islam hakuna yeyote kati yao aliyetambuka mwanzo wa karne ya kumi na nne katika kuutaja kuwa ndio zama za ujaji wa Masihi Mau'udi. Sasa kitabia swali hili linazuka hapa kwamba kulikuwa na haja gani ya kumtuma Masihi Mau'udi kutoka ndani ya umati huu? Jibu lake ni kwamba Mwenyezi Mungu Ameahidi ndani ya Kurani Tukufu kwamba Mtume[saw] katika mwanzo na mwisho wa unabii wake atafanana na nabii Musa[as]. Hivyo mshabaha huo mmoja ulikuwa katika zama za mwanzo ambazo ni zama za Mtume[saw], na mwingine ni katika zama za mwisho. Hivyo mshabaha wa kwanza umethibitika hivi kwamba kama vile Mungu

hatimaye Alimpa Musa ushindi juu ya Firauni na jeshi lake vivyo hivyo hatimaye Alimpa Mtume[saw] ushindi juu ya Abu Jahli aliyekuwa Firauni wa zama hizo, na jeshi lake, na kwa kuwaangamiza wote hao Akaistawisha Islam katika bara Arabu na kutokana na msaada huu wa Mungu bishara hii ikatimia:

اِنَّآ اَرْسَلْنَآ اِلَيْكُمْ رَسُوْلًا ۙ شَاهِدًا عَلَيْكُمْ
كَمَآ اَرْسَلْنَآ اِلٰى فِرْعَوْنَ رَسُوْلًا ﴿١٦﴾[6]

Na katika zama za mwisho kuna mshabaha huu kwamba katika zama za mwisho za umati wa Musa[as] alimtuma nabii mmoja ambaye alipingana na jihadi na hakuwa na uhusiano wowote na vita za kidini bali kusamehe kulikuwa ni mafundisho yake. Na alikuja katika wakati ambao hali za khulka za wana wa Israeli zilikuwa zimeshaharibika mno na uharibifu mwingi ulikuwa umetokea katika mwenendo wao, na ufalme wao ulikuwa ukiwaponyoka, nao walikuwa chini ya utawala wa Kirumi, naye alidhihiri barabara kwenye karne ya kumi na nne baada ya Musa[as], na silsila ya unabii wa Kiisraeli ikawa imeishia kwake naye alikuwa tofali la mwisho la unabii wa Kiisraeli.

[6] Hakika Sisi Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni. *Al-Muzzammil*, 73:16

Hali kadhalika katika zama za mwisho za Mtume[saw] amemtuma mwandishi huyu katika hali na sifa ya Masihi mwana wa Mariamu[as], na desturi ya jihadi Ameiondolea katika zama zangu kama ilivyopashwa habari hapo kabla kuwa katika zama za Masihi Mau'udi jihadi itasitishwa. Hali kadhalika mimi nimepewa mafundisho ya kusamehe. Na nimekuja katika wakati ambao hali ya ndani ya Waislamu wengi ikiwa ilishaharibika kama ya Wayahudi, na baada ya kutoweka kwa hali ya kiroho ikawa kwao ilibakia tu kuabudu mila na desturi. Na mambo hayo mapema yaliashiriwa ndani ya Kurani Tukufu, kama vile katika sehemu fulani Kurani Tukufu imetumia kwa ajili ya Waislamu wa zama za mwisho neno ililotumia kwa Wayahudi, yaani kasema:

فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُوْنَ [7]

ambayo maana yake ni kwamba nyinyi mtapewa ukhalifa na usultani, lakini katika zama za mwisho mtanyang'anywa usultani huo kutokana na matendo yenu mabaya kama walivyonyang'anywa Wayahudi. Halafu ndani ya Sura Nuur, Anaashiria kwa uwazi

---

[7] Na Aone jinsi mtakavyofanya. *Al-A'raaf*, 7:130

kwamba jinsi makhalifa wa kila aina walivyopita miongoni mwa wana wa Israeli, basi aina zote hizo zitakuwemo pia ndani ya makhalifa wa umati huu. Hivyo miongoni mwa makhalifa wa Kiisraeli, Hadhrat Isa[as] alikuwa ni Khalifa ambaye hakunyanyua upanga wala kupigana jihadi. Basi umati huu pia umepewa Masihi Mau‘udi wa aina hiyo hiyo. Itazameni aya hii:

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ كَمَا
اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۪ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِي ارْتَضٰى لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا ؕ يَعْبُدُوْنَنِيْ لَا يُشْرِكُوْنَ بِيْ شَيْـًٔا ؕ وَمَنْ
كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿۵۶﴾[8]

Katika aya hii maneno

كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۪

[8] Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. *An-Nuur*, 24:56

yapaswa kuzingatiwa, kwa sababu kutokana na hayo inafahamika kuwa silsila ya ukhalifa wa Muhammad[saw] inafanana na silsila ya ukhalifa wa Musa[as], na kwa kuwa mwishoni mwa ukhalifa wa Musa[as] alitokea nabii wa aina hii, yaani nabii Isa[as], aliyekuja mwanzoni mwa karne ya kumi na nne baada ya Musa na hakupigana vita yoyote wala jihadi, hivyo ilikuwa ni lazima Khalifa wa mwisho wa silsila ya Muhammad[saw] awe pia wa shani hiyo hiyo.

Hali kadhalika ndani ya Hadithi sahihi pia ilitajwa kuwa katika zama za mwisho Waislamu wengi watafanana na Wayahudi na hata ndani ya sura ya Fatiha pia iliashiriwa haya haya, kwa sababu humo imefundishwa dua hii kwamba Ee Mungu utulinde tusiwe kama Wayahudi wale waliokuwepo wakati wa Hadhrat Isa[as] na walikuwa wapinzani wake, ambao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iliwateremkia humu humu duniani. Na hii ni desturi ya Mwenyezi Mungu kwamba Mwenyezi Mungu Atoapo agizo lolote kwa watu fulani au Awafundishapo dua yoyote ile basi mradi wake unakuwa huu kwamba baadhi ya watu miongoni mwao watakumbwa na dhambi hiyo waliyokatazwa. Hivyo, kwa kuwa mradi wa aya:

غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ [9]

unawahusu Wayahudi wale waliokuwepo katika zama za mwisho za umati wa Musa, yaani katika wakati wa Hadhrat Masihi, kwa sababu ya kutomkubali Hadhrat Masihi[as] wakawa lengo la ghadhabu ya Mungu, hivyo katika aya hii, kulingana na suna iliyotajwa, kuna bishara kwamba hata katika zama za mwisho za umati wa Muhammad[saw], Masihi Mau'udi atadhihiri toka katika umati huu huu, na baadhi ya Waislamu wakifanya upinzani dhidi yake watajifananisha na Wayahudi wale waliokuwa katika zama za Hadhrat Masihi. Hili si jambo la kutolewa upingamizi kwamba kama Masihi ajaye alitakiwa atokane na umati huu huu sasa kwa nini katika Hadithi ameitwa jina Isa? Kwa sababu desturi ya Mungu hutokea hivi kwamba mmoja hupewa jina la mwingine kama vile katika Hadithi Abu Jahli alipewa jina la Firauni na Hadhrat Nuh akapewa jina la Adam wa Pili na Yohana akapewa jina la Eliya. Hii ni ile desturi ya Mungu ambayo hakuna yeyote yule aikataaye. Na Mwenyezi Mungu Amempa Masihi ajaye mfanano

---

[9] *Al-Faatiha*, 1:7

huu na Masihi aliyepita kwamba Masihi wa awali, yaani Hadhrat Isa[as], alidhihiri kwenye karne ya kumi na nne baada ya Hadhrat Musa[as], na halikadhalika Masihi wa mwisho amedhihiri kwenye karne ya kumi na nne baada ya Mtume[saw] katika wakati ambao utawala wa Kiislamu nchini India ulikuwa ukitokomea na ilikuwa ni zama za utawala wa Kiingereza, kama vile Hadhrat Masih[as] pia alidhihiri katika wakati ambao utawala wa Kiisraeli ulikuwa umekwisha na Wayahudi wakawa wameshakuwa chini ya utawala wa Warumi. Na kwa ajili ya Masihi Mau'udi wa umati huu kuna mfanano mwingine na Hadhrat Isa[as], nao ni huu kwamba Hadhrat Isa[as] hakutokana na wana wa Israeli kikamilifu bali alikuwa akiitwa Mwisraeli kwa sababu tu ya mama yake. Nami pia baadhi ya mabibi zangu walitokana na ukoo wa Masharifu (vizazi vya Mtume[saw]) ingawa baba hatokani na ukoo huo wa masharifu. Na Mungu Alivyopenda kwa ajili ya Hadhrat Isa[as] kwamba Mwisraeli yeyote hakuwa baba ya Hadhrat Masihi Mwisraeli, ndani yake mlikuwa na siri hii kwamba Mwenyezi Mungu Aliwakasirikia sana Waisraeli kutokana na wingi wa madhambi. Hivyo, Akawaonyesha ishara hii kwa kuwatanabahisha

kwamba miongoni mwao Alimwumba mtoto mmoja kwa njia ya mama tu bila ya kushirikiana na baba. Kana kwamba Hadhrat Masihi[as] alibakiwa na sehemu moja tu kati ya sehemu mbili za mwili wa Kiisraeli. Hii ilikuwa inaashiria kwenye jambo hili kwamba hata yule Nabii atakayekuja hatatokana nao kabisa. Sasa kwa kuwa dunia inakaribia kwisha, ndio sababu hata katika kuzaliwa kwangu hivi kuna ishara, nayo ni hii kwamba Kiama kimekaribia, nacho ndicho kitakachozimaliza ahadi za Ukhalifa wa Kikureshi. Ilmuradi, kwa ajili ya kukamilisha mshabaha wa Musa na Muhammad[saw] kulikuwa na haja ya Masihi Mau'udi ambaye angedhihiri pamoja na masharti yote hayo. Kama vile silsila ya Islam ilivyoanzia kwa yule aliye mfano wa Musa, vivyo hivyo silsila hiyo ilivyotakiwa imalizikie kwa yule aliye mfano wa Isa, ili mwisho ufanane na mwanzo. Hivyo, huu pia ni uthibitisho wa ukweli wangu, lakini kwa watu wale wanaotafakari kwa kumcha Mungu. Mungu Awarehemu Waislamu wa zama hizi, kwani mambo mengi ya itikadi yao yameshapita mpaka wa dhuluma na kukiuka uadilifu. Wanasoma ndani ya Kurani Tukufu kwamba Hadhrat Isa[as] ameshakufa na kisha wanamfahamu kuwa yu hai. Halikadhalika wanasoma

ndani ya Kurani Tukufu katika sura "An-Nuur" kwamba Makhalifa wote wajao watatoka ndani ya umati huu huu na halafu wanamteremsha Hadhrat Isa[as] toka mbinguni. Na wanasoma ndani ya Sahih Bukhari na Muslim kuwa yule Isa atakayekuja kwa ajili ya umati huu atatokana na umati huu huu, halafu wanamsubiri Isa wa Kiisraeli. Na wanasoma ndani ya Kurani Tukufu kuwa Isa hatakuja tena duniani, na juu ya kuelewa hii bado wanataka kumleta tena duniani, na juu ya yote hayo wanadai kuwa Waislamu. Na wanasema kwamba Hadhrat Isa[as] alinyanyuliwa mbinguni na kiwiliwili chake, lakini hawatoi jibu kwamba kwa nini alinyanyuliwa. Ugomvi wa Wayahudi ulihusiana tu na kunyanyuliwa kiroho. Hao walikuwa na dhana kuwa roho ya Hadhrat Isa[as] haikunyanyuliwa mbinguni kama wenye imani kwa kuwa alifishwa msalabani, na yule afishwaye msalabani huwa amelaaniwa, yaani roho yake huwa hainyanyuliwi mbinguni kwa Mungu. Na Kurani Tukufu ilikuwa itoe tu uamuzi wa ugomvi huu tu kama inavyodai Kurani Tukufu kuwa inayadhihirisha makosa ya Wayahudi na Wakristo na kutoa uamuzi wa kuhitilafiana kwao. Na ugomvi wa Wayahudi ulikuwa huu kwamba Isa Masihi hakuwa miongoni

mwa waaminio na wala hakuokoka na wala roho yake haikupaa kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, jambo la kuamuliwa lilikuwa kwamba je Masihi Isa[as] alikuwa ni mwaminio na Nabii mkweli wa Mungu au la? Na roho yake ilinyanyuliwa kwa Mwenyezi Mungu kama waaminio wengine au la? Hili ndilo ambalo Kurani ilitakiwa kuliamua. Hivyo kama maana ya aya:

بَلْ رَّفَعَهُ اللّٰهُ اِلَيْهِ[10]

ndiyo hii kwamba Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Hadhrat Isa[as] pamoja na mwili wake katika mbingu ya pili, basi kwa kitendo hicho ni uamuzi gani uliotolewa katika jambo hilo lenye hitilafu? Inakuwa kana kwamba Mungu Hakulielewa jambo hilo lenye hitilafu, na hivyo Katoa uamuzi ambao haukuhusiana hata kidogo na dai la Wayahudi.

Halafu ndani ya aya imeandikwa kwa uwazi kuwa rufai ya Isa kulikuwa ni kwa Mungu, wala haikuandikwa kanyanyuliwa kwenye mbingu ya pili. Je, Mwenyezi Mungu Ameketi kwenye mbingu ya pili? Au kwa ajili ya kuokoka na kuwa na imani ni

[10] Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Kwake. *An-Nisaa*, 4:159

lazima pia kuwa mwili nao unyanyuliwe? Na jambo la ajabu ni hili kwamba ndani ya aya

بَلۡ رَّفَعَهُ اللّٰهُ اِلَیۡهِ[11]

hata hamkutajwa neno mbinguni, bali aya hii yamaanisha tu kwamba Mungu Alimnyanyua Kwake. Sasa hebu semeni kwamba je Hadhrat Ibrahim[as], Hadhrat Ismail[as], Hadhrat Isihaka[as], Hadhrat Yakubu[as], Hadhrat Musa[as] na Hadhrat Muhammad [saw], Mungu Apishe mbali, walinyanyuliwa upande mwingine na sio kwa Mungu?

Mimi hapa nasema kwa kukazania kwamba kumfahamu Hadhrat Masihi pekee kuwa ndiye anahusika na aya hii yaani kumhusisha yeye pekee na kunyanyuliwa kwa Mungu na kuwaweka manabii wengine nje ya hiyo, hilo ni neno la kufuru, hakuna kufuru nyingine yoyote itakayokuwa kubwa zaidi ya hiyo. Kwa sababu kutokana na maana hizo, manabii wote hawakunyanyuliwa isipokuwa Hadhrat Isa[as], ilhali Mtume[saw] alipokuja toka Miraji alitoa ushahidi pia wa kunyanyuliwa kwao.

---

[11] Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Kwake. *An-Nisaa*, 4:159

Na kumbukeni pia kwamba kutajwa kwa rufai ya Hadhrat Isa[as] ilikuwa tu kwa ajili ya kuwatanabahisha Wayahudi na kuondoa shutuma, waila rufai hii ni kawaida kwa manabii na mitume wote na waaminio wote, na baada ya kufa kila mwaminio hunyanyuliwa. Hivyo, ndani ya aya:

هٰذَا ذِكْرٌ ؕ وَاِنَّ لِلْمُتَّقِيْنَ لَحُسْنَ مَاٰبٍ ۙ جَنّٰتِ عَدْنٍ مُّفَتَّحَةً لَّهُمُ الْاَبْوَابُ ۚ[12]

kuna ishara kwenye kurufaishwa huku. Lakini kafiri huwa harufaishwi, na aya:

لَا تُفَتَّحُ لَهُمْ اَبْوَابُ السَّمَآءِ[13]

inaashiria kwenye jambo hilo hilo. Naam, wale watu wa kabla yangu waliokosea katika jambo hili wao wamesamehewa kosa hilo, kwa sababu wao hawakukumbushwa, wao hawakufahamishwa maana ya kweli ya maneno ya Mungu. Lakini mimi nimewakumbusheni na kuwafahamisheni maana zilizo sahihi kabisa. Kama mimi nisingekuja basi kungekuwepo na udhuru wa kufuata mila kwa ajili ya

[12] Huu ni ukumbusho! na kwa yakini wamchao Mungu mahali pao pa kurudia patakuwa pazuri. Bustani za kukaa milele zilizofunguliwa milango kwa ajili yao. *Saad*, 38:50-51

[13] Hawatafunguliwa milango ya mbingu. *Al-A'raaf*, 7:41

kosa hilo, lakini sasa hakuna udhuru wowote uliobakia. Mbingu imetoa ushahidi kwa ajili yangu na ardhi pia, na baadhi ya mawalii wa umati huu wametoa ushuhuda wangu kwa kulitaja jina langu na la makazi yangu kwamba ndiye huyo huyo Masihi Mau‘udi. Na baadhi ya watoa ushuhuda walishaiaga dunia miaka thelathini kabla ya kudhihiri kwangu kama vile nilivyokwisha chapisha ushuhuda wao. Na hata katika zama hizi baadhi ya mawalii waliokuwa na malaki ya wafuasi walinisadikisha baada ya kupata wahyi toka kwa Mungu na kumsikia Mtume[saw] katika ruya. Na hadi sasa maelfu ya ishara zimeshadhihirika toka kwangu. Na manabii watakatifu wa Mungu waliukadiria wakati wangu na zama zangu. Na kama mtafakari basi hata mikono yenu, miguu yenu na mioyo yenu pia inatoa ushuhuda kwangu. Kwa sababu kasoro zimepita kiasi na watu wengi wameusahau hata utamu wa imani. Na kasoro, unyonge, kosa, upotofu, kuiangukia dunia na kiza kinachoikumba kaumu hii, hali hii kwa asili yahitaji kwamba mtu mmoja asimame na kuwasaidia. Na juu ya hayo hadi sasa naitwa Dajjali. Kaumu ile ndiyo yenye bahati mbaya namna gani ambayo katika hali yake ya hatari kiasi hiki atumwe Dajjali kwao. Hiyo

kaumu ndiyo yenye bahati mbaya kiasi gani ambayo katika wakati wake wa maangamio ya ndani wapatiwe maangamio mengine toka mbinguni. Na wanasema kwamba mtu huyu ni malauni, hana imani. Maneno haya haya yalisemwa kwa Hadhrat Isa[as] pia, na Mayahudi walionajisika hadi leo wanaendelea kusema hayo. Lakini mnamo siku ya Kiama wale watakaoionja Jahanamu watasema:

مَا لَنَا لَا نَرٰى رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُمْ مِّنَ الْأَشْرَارِ ﴿٦٣﴾ [14]

Dunia daima imewafanyia uadui wale waliotumwa na Mungu, kwani kuipenda dunia na kuwapenda waliotumwa na Mungu kamwe hakuwezi kujumuika katika sehemu moja. Na kama nyinyi msingeipenda dunia mngeniona; lakini sasa hamuwezi kuniona.

Halafu mbali na hayo ikiwa jambo hili ni sahihi kwamba aya ya:

بَلْ رَّفَعَهُ اللّٰهُ إِلَيْهِ [15]

[14] Imekuwaje, hatuwaoni watu tuliokuwa tukiwahesabu katika waovu? *Saad*, 38:63

[15] Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Kwake. *An-Nisaa*, 4:159

maana yake ni hii hii kuwa Hadhrat Isa[as] alinyanyuliwa kwenye mbingu ya pili, basi inafaa kuonyesha kuwa uamuzi wa jambo lenyewe la mzozo umetajwa katika aya ipi? Wayahudi ambao hadi sasa wako hai na wapo, wao wanazikataa maana hizi za kurufaishwa kwa Isa kwamba yeye, Mungu Apishe mbali, hakuwa mwaminio wala mkweli na roho yake haikurufaishwa kwa Mungu. Kama mna shaka nendeni mkawaulize wanazuoni wa Wayahudi kwamba wao kutokana na kifo cha msalaba hawafikii katika uamuzi huu kwamba kwa kifo hiki roho pamoja na mwili haiendi mbinguni. Bali kwa kauli moja wanasema kwamba yule mtu aliyeuawa kwa njia ya msalaba huyo amelaaniwa, huwa harufaishwi kwa Mungu. Na hii hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu Amekikanusha kifo cha Hadhrat Isa[as] msalabani na kusema:

وَمَا قَتَلُوْهُ وَمَا صَلَبُوْهُ وَلٰكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ ط[16]

Ndani ya aya pamoja na *salabuuhu* Ameongeza neno *Qataluuhu* ili kuashiria kwamba kutundikwa tu msalabani sio sababu ya laana, bali sharti ni hili

16 Hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti) An-Nisaa, 4:158

kwamba atundikwe pia msalabani na kwa nia ya kuua miguu yake pia ivunjwe na pia auawe, ndipo kifo hicho kitasemwa kuwa ni kifo cha malauni. Lakini Mungu Alimwokoa Hadhrat Isa[as] na kifo hiki. Yeye alitundikwa msalabani lakini kifo chake hakikutokana na msalaba. Naam, ndani ya mioyo ya Wayahudi iliingizwa shaka hii kana kwamba amekufa msalabani. Na Wakristo nao walidanganyika hivyo hivyo. Naam, wao wakadhani kwamba alifufuka baada ya kufa. Lakini jambo lenyewe lilikuwa hivi tu kwamba alizimia kutokana na mateso ya msalabani, na hii hii ndiyo maana ya: شُبِّهَ لَهُمْ. Juu ya tukio hilo tiba ya "Marhamu ya Isa" ni ushahidi mmoja wa ajabu, ambayo tangu karne nyingi imekuwa inaandikwa katika vitabu vya tiba vya Waibrania, Warumi, Wayunani na Waislamu ambayo katika kuielezea wameandika kwamba dawa hii ilitengenezwa kwa ajili ya Hadhrat Isa[as]. Ilmuradi fikara hizi ni za aibu mno kwamba Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Hadhrat Masihi pamoja na mwili wake mbinguni, kana kwamba Alikuwa Anawaogopa Wayahudi wasije kumkamata. Wale ambao hawakuwa na habari za mzozo wenyewe ndio waliozieneza fikira hizi. Na fikara kama hizo

zamwondolea Mtume[saw] heshima. Kwa sababu makafiri wa Kikureish kwa msisitizo mkubwa kabisa walimuomba muujiza huu kwamba upae mbinguni mbele yetu na uteremke na kitabu toka mbinguni, basi hapo sote tutaamini, nao wakapewa jibu hili:

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيْ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَّسُوْلًا ۝٩٤ ع [17]

yaani, mimi ni mwanadamu tu, na Mwenyezi Mungu ni Mtakatifu kutenda kinyume na ahadi yake kwa kumnyanyua mwanadamu yeyote mbinguni ilhali Alishatoa ahadi kuwa wanadamu wote watapitisha maisha yao hapa ardhini, lakini Mungu Akamnyanyua Hadhrat Masih[as] pamoja na mwili wake mbinguni bila kuizingatia ahadi ile, kama Alivyosema:

فِيْهَا تَحْيَوْنَ وَفِيْهَا تَمُوْتُوْنَ وَمِنْهَا تُخْرَجُوْنَ [18]

Baadhi yao wanadhani kuwa hatuna haja ya kumwamini Masihi Mau'udi yeyote, na wanasema kwamba ingawa tumekubali kuwa Hadhrat Isa[as] amekufa, lakini maadam sisi ni Waislamu na tunasali

---

[17] Sema: Mola wangu ni Mtakatifu! Mimi siye ila ni mtu tu, Mtume. *Banii Israaiil*, 17:94

[18] Akasema: Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo. *Al-A'raaf*, 7:26

na kufunga na kufuata maagizo ya Kiislamu, sasa tena tuna haja gani na mwingine? Lakini ikumbukwe kwamba watu wenye mawazo haya wako kwenye makosa sana. Kwanza wanawezaje kudai kuwa ni Waislamu ilhali hawaamini agizo la Mungu na Mtume[saw] Agizo lilikuwa ni kwamba atakapodhihiri huyo Imam Mau'udi basi mumkimbilie bila kusita, na hata kama itabidi kutambaa juu ya theluji, hata hivyo jifikisheni kwake. Lakini kinyume chake sasa inadhihirishwa hali ya kutojali. Je, hii ndiyo Islamu? Na hii ndio imani juu ya Uislamu? Na sio kiasi hicho tu, bali matusi makubwa makubwa yatolewa na anaitwa kafiri na kupewa jina la Dajjali. Na yule mtu anayeniudhi hujidhani amefanya jambo la thawabu kubwa, na yule anayeniita "mwongo, mwongo," hufahamu kuwa amemfurahisha Mungu.

Enyi watu, mliokuwa mmepewa mafundisho ya subira na ucha Mungu, nani amewafundisheni papara na dhana mbaya? Ni ishara ipi ambayo Mungu Hakuidhihirisha? Na ni dalili gani ambayo Mungu Hakuitoa? Lakini nyinyi hamkukubali, na mkajasiri kuyapiga chenga maagizo ya Mungu. Niwafananishe na nani watu wenye hila wa zama hizi? Wanafanana na mwenye hila yule ambaye akiyafumba macho yake

mchana kweupe anasema jua li wapi? Ee unayeidanganya nafsi yako! Kwanza fumbua jicho lako, ndipo utaliona jua. Ni rahisi kumsema mtume wa Mungu kuwa kafiri, lakini ni vigumu kumfuata ndani ya njia nyembamba za imani. Ni rahisi kumsema Dajjali yule aliyetumwa na Mungu, lakini ni jambo gumu kuingia kupitia kwenye mlango mwembamba sawa na mafundisho yake. Yeyote asemaye: mimi simjali Masihi Mau'udi, basi huyo haijali imani. Watu wa aina hiyo huwa hawaijali imani ya kweli na wokovu na utakaso wa kweli. Kama wafanye uadilifu kidogo tu na kujitazama hali zao za ndani, basi watafahamu kuwa bila ya yakini hii mpya ambayo huteremka toka mbinguni kupitia kwa mitume na manabii wa Mungu, sala zao ndio kwa sabbu ya kuifuata mila na mazoea tu, na saumu zao ni kushinda tu na njaa. Ukweli hasa ni huu kwamba hakuna mwanadamu yeyote kwa kweli awezaye hasa kupata kujiokoa katika dhambi, na wala hawezi kumpenda Mungu kikweli, na wala hawezi kumwogopa kama ipasavyo bila ya kupata utambuzi wake kutokana na fadhili na rehema yake na bila ya kupata nguvu toka Kwake. Na jambo hili ni dhahiri kabisa kwamba kila hofu na kila penzi hupatikana

kutokana na utambuzi tu. Vitu vyote vya duniani avielekeavyo mwanadamu na kuvipenda au vile aviogopavyo na kuvikimbia mbali, hali zote hizi huzalika ndani ya moyo wa mwanadamu baada tu ya kupata utambuzi. Naam, hii ni kweli kwamba utambuzi hauwezi kupatikana bila ya kuwepo fadhili ya Mungu na wala hauwezi kufaa bila ya kuwepo kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu. Na utambuzi huja kwa njia ya fadhili, ndipo kwa njia ya utambuzi mlango mmoja wa kuuona na kuutafuta ukweli hufunguka, na hapo mara kwa mara kwa fadhili tu mlango huo huendelea kufunguka na huwa haufungiki. Ilmuradi, utambuzi hupatikana kwa njia ya fadhili na halafu hubakia kwa njia ya fadhili tu. Fadhili huufanya utambuzi kuwa safi mno na wenye kung'aa na huyaondoa mapazia katikati na huliondolea mbali vumbi la nafsi *ammaara* (inayoshawishi kwenye maovu) na huipa roho nguvu na uhai na kuitoa nafsi *ammaara* toka kwenye 'gereza' ya mwelekeo wa maovu na kuitakasa na uchafu wa matamanio mabaya na kuitoa nje kutoka katika mafuriko makali ya jadhba za nafsi. Hapo ndipo mabadiliko hupatikana ndani ya mwanadamu naye anayachukia kitabia maisha machafu, kisha baadaye harakati ya kwanza

inayozalika ndani ya roho kwa njia ya fadhili huwa ni dua. Msifikirie kwamba sisi pia kila siku twaomba dua na sala zote tunazosali huwa ni dua, kwani dua ile inayozalika baada ya kupata utambuzi na kwa njia ya fadhili huwa ya namna nyingine na hali tofauti. Huwa ni kitu chenye kuhilikisha, huwa ni moto wenye kulainisha, huwa ni nguvu ya kisumaku inayoivuta rehema, huwa ni mauti lakini hatimaye yahuisha, huwa ni mafuriko makali lakini mwishoni yanageuka kuwa safina. Kila jambo lililoharibika hutengenezeka kwa hiyo, na kila sumu kwayo hugeuka mwishowe kuwa dawa inayozuia dhara ya sumu.

Wamebarikiwa wafungwa wale waombao dua bila ya kuchoka, kwani siku moja watafunguliwa. Wamebarikiwa vipofu wale wasio wavivu katika kuomba dua, kwani siku moja wataanza kuona. Wamebarikiwa wale waliomo makaburini wakifanya maombi kuomba msaada wa Mungu, kwa sababu siku moja watatolewa nje kutoka makaburini.

Mmebarikiwa ninyi msipochoka hata kidogo kuomba dua, na roho zenu zinayeyuka kwa ajili ya maombi na macho yenu yanatiririsha machozi na kuzalisha moto fulani ndani ya vifua vyenu na kuwapelekeni ndani ya

vyumba vyenye kiza na misitu pasipo watu kwa ajili ya kuipata ladha ya kuwa upwekeni na kuwafanyeni kuwa wenye kukosa utulivu, wenye kelemewa na mapenzi na kuwa kama mliochanganyikiwa, kwani hatimaye mtafadhiliwa. Yule Mungu tunayeitia Kwake ni Mkarimu na Mrahimu mno, Mwenye haya, Mkweli, Mwaminifu, Mwenye kuwahurumia wanyonge. Basi nanyi pia kuweni waaminifu na ombeni dua kwa ikhlasi na uaminifu kamili, hivyo Yeye Atawarehemuni. Jitengeni na vurugu za dunia, na magomvi ya nafsi msiyafanya kuwa ya kidini. Jichagulieni ushinde, na kubalini kushindwa ili mkawe warithi wa maushindi makubwa makubwa. Mungu Atawaonyesha mwujiza waombao dua, na waombao watapewa neema ya kimwujiza. Dua hutoka kwa Mungu na kuelekea huko huko Kwa Mungu. Kutokana na dua Mungu Anakuwa karibu kama vile roho yenu ilivyo karibu nanyi. Neema ya kwanza ya dua ni kwamba mabadiliko matakatifu huzalika ndani ya mwanadamu, halafu kutokana na mabadiliko haya Mungu pia Hufanya mabadiliko katika sifa Zake. Na sifa Zake si zenye kubadilika lakini kwa ajili ya mwenye kubadilika kunakuwa na mdhihirisho mmoja tofauti ambao dunia haiufahamu,

kana kwamba Yu Mungu mwingine ilhali hakuna Mungu mwingine yeyote yule, lakini mdhihirisho mpya unamdhihirisha kwa namna mpya. Ndipo katika shani ya mdhihirisho huo makhsus Humtendea yule aliyebadilika yale ambayo Hawatendei wengine. Huu huu ndio ule mwujiza.

Ilmuradi, dua ni dawa ile inayoufanya ukufi wa vumbi (mtu) kuwa dhahabu, nayo ni maji yale yasafishayo taka za ndani. Kwa dua hiyo roho huyeyuka na kutiririka kama maji hadi kwenye kizingiti cha Mwenyezi Mungu. Husimama mbele ya Mwenyezi Mungu na pia huinama na husujudu pia, na kivuli chake ni sala ile iliyofundishwa na Islam. Na kusimama kwa roho ni kwamba hiyo inaonyesha juhudi kwa kuvumilia kila aina ya msiba kwa ajili ya Mungu na kutii amri. Na rukuu yake yaani kuinama ni hii kwamba ikiacha mapenzi na mahusiano yote inaelekea kwenye Mungu na kuwa kwa Mungu. Na sijida yake ni hii kwamba ikianguka kwenye kizingiti cha Mungu inapoteza kabisa mawazo yake na kujifuta kabisa. Hii ndiyo sala inayounganisha kwa Mungu, na sheria ya Kiislamu imeonyesha taswira yake ndani ya sala ya kawaida ili sala ile ya kimwili ielekeze kwenye sala ya kiroho, kwa sababu Mwenyezi

Mungu Ameliumba umbile la mwanadamu hivi kwamba ni lazima athari ya roho inakuwa juu ya mwili na athari ya mwili inakuwa juu ya roho. Roho yenu inapohuzunika, basi machozi yanatirikika kutoka kwa macho pia, na furaha inapokuwepo ndani ya roho, basi bashasha inaonekana usoni kiasi ya kwamba wakati mwingine mtu anaanza kucheka. Vivyo hivyo mwili unapofikiwa na shida na maumivu basi roho pia hushiriki katika hayo, na mwili unapofurahishwa na upepo baridi, basi roho pia inachukua sehemu kiasi fulani kutoka hiyo. Hivyo, kusudio la ibada za kimwili ni hili kwamba kutokana na mahusiano kati ya roho na mwili ipatikane harakati ndani ya roho ya kuelekea kwa Mungu Aliye Mmoja, nayo ijishughulishe katika kusimama kiroho na kusujudu kiroho. Kwani mwanadamu anahitaji kufanya jitihada kwa ajili ya maendeleo, na hii pia ni aina fulani ya jitihada. Hii ni dhahiri kwamba kama kuna vitu viwili vilivyoshikamana kwa pamoja, tutakapokinyanyua kimojawapo, basi kwa kukinyanyua hicho kile kitu kingine kilichoshikamana nacho pia husogea. Lakini katika kusimama na kuinamna na kusujudu kimwili tu hakufai kitu isipofanywa juhudi hii kwamba roho nayo kwa namna

yake ipate hisa katika kusimama na kurukuu na kusujudu. Na kupata hisa hii kunautegemea utambuzi, na utambuzi unaitegemea fadhili. Na Mungu tangu kale na tangu Alipomwumba mwanadamu Alianzisha suna hii kwamba kwanza Yeye kwa fadhili yake kubwa Humutilia roho mtakatifu yule Amtakaye, halafu kwa msaada wa roho mtakatifu huzalisha ndani yake mapenzi Yake na kumpatia ikhlasi na uimara, na huuimarisha utambuzi wake kwa ishara nyingi sana na kuuondolea mbali udhaifu wake kiasi ya kwamba anakuwa tayari kwelikweli kuyatoa maisha yake katika njia Yake. Na anakuwa na uhusiano wake na Dhati Yule, Asiye na mwanzo, usiokatika kiasi ya kwamba uhusiano huo hauwezi kutoweka kwa msiba wowote ule na hakuna upanga wowote uwezao kuukata uhusiano huo. Na mapenzi hayo hayana tegemeo lolote la muda, si tamaa ya Pepo wala hofu ya Jahanamu wala starehe za dunia na wala mali na utajiri, bali ni uhusiano usiofahamika ambao ni Mungu tu Ndiye Aujuaye. Na la ajabu zaidi ni kwamba hata yule aliyeshikwa na haya mapenzi naye hawezi kufika kwenye kiini cha uhusiano huu kwamba ni kwa nini na kwa tashi lipi na kwa namna gani, kwa sababu uhusiano huo ni wa tangu azali.

Uhusiano huo hautokani na utambuzi, bali utambuzi huja baadaye ambao huuangazia uhusiano huo, ni kama vile moto ambao tangu mwanzo umo ndani ya jiwe, lakini kutoka kwa jiwe gumu lile la *flint* moto huanza kutoka kwa msuguano. Na ndani ya mtu wa aina hii, kwa upande mmoja kunakuwepo na mapenzi ya dhati ya Mwenyezi Mungu na kwa upande mwingine kunakuwepo pia na upendo wa kuwahurumia na kuwarekebisha wanadamu. Hii ndiyo sababu, kwa upande mmoja mwungano wake na Mungu unakuwa wa namna ambavyo yeye anadumu kuvutika Kwake, na kwa upande mwingine uhusiano wake na wanadamu unakuwa hivi kwamba huzivutia upande wake silika zao za asili zilizo tayari kama vile jua linavyozivuta tabaka zote za ardhi upande wake na lenyewe pia linavutika upande mmoja. Hii hii ndio inakuwa hali ya yule mtu. Katika istilahi ya Islam watu wa aina hii huitwa kuwa Nabii, Rasul na Muhaddath nao hupewa heshima ya kuzungumza na Mwenyezi Mungu, na miujiza hudhihirika mikononi mwao, na dua zao nyingi hukubaliwa, na ndani ya dua zao hupata kwa wingi majibu toka kwa Mungu. Baadhi ya majahili wasema hapa kwamba hata sisi mbona twapata ndoto za

kweli; wakati mwingine hata dua yakubaliwa na wakati mwingine hata ilhamu twapata, basi kuna tofauti gani kati yetu na mitume? Hivyo, kwa rai yao manabii ni watu wenye hila au waliodanganyika ambao huona fahari kwa jambo dogo tu na hamna tofauti yoyote kati yao na watu wengine. Hayo ni mawazo ya majigambo ambayo kwayo watu wengi siku hizi wanaangamia. Lakini kwa ajili ya mtafuta ukweli kuna jibu safi la wasiwasi huo, nalo ni hili kwamba bila shaka ni kweli kuwa Mungu Amelichagua kundi moja kwa fadhili Zake makhsus pamoja na rehema na kuwapa sehemu kubwa ya neema Zake za kiroho, ndio sababu ingawaje maadui kama hao na vipofu wakawakataa manabii, lakini hata hivyo manabiiwakaendelea kupata ushindi juu yao, na nuru yao ya kimwujiza daima iliendelea kudhihirika kwa namna ambavyo hatimaye wenye akili wakalazimika kuamini kuwa kuna tofauti kubwa kati yao (manabii) na wengine. Kama vile ilivyo dhahiri kwamba masikini anayeombaomba pia anazo dirhamu kiasi kidogo na mfalme pia anayo hazina ziliyojaa dirhamu, lakini yule masikini hawezi kusema kuwa mimi niko sawa na mfalme. Au kwa mfano ndani ya mdudu fulani kuna mwanga ambao humetemeta

wakati wa usiku na ndani ya jua pia kuna mwanga, lakini mdudu hawezi kusema kuwa mimi niko sawa sawa na jua. Na baadhi ya mbegu za ruya, kashfi na ilhamu ambazo Mwenyezi Mungu Amezipanda ndani ya nafsi za watu wa kawaida ni kwa sababu hii tu kwamba waweze kuwatambua manabii kwa uzoefu wao huo na kwa njia hii pia hoja itimie juu yao na usibakie udhuru wowote.

Na halafu sifa makhsus iliyomo ndani ya waja wateule wa Mwenyezi Mungu ni hii kwamba wao ni watu wenye athari na mvuto, nao hutumwa duniani kuja kustawisha vizazi vya kiroho. Na kwa kuwa wao huongoza kwa yakini na huziondoa njiani pazia zenye kiza za viumbe, kwa hiyo utambuzi wa kweli wa Mungu na mapenzi ya kweli ya Mungu na utawa na ucha Mungu wa kweli na shauku na utaamu huzalika mioyoni kupitia kwao, na kuvunja nao uhusiano inakuwa kama vile tawi lijikate toka kwenye mti wake. Na katika mahusiano hayo kuna sifa fulani makhsus kwamba kwa kuweka tu uhusiano — kwa sharti ya mnasaba — ustawisho wa kiroho huanza. Na kwa kukata tu uhusiano, vumbi huanza kuja kwenye hali ya imani. Hivyo, hili ni wazo la kiburi kabisa kwamba mtu aseme mimi sina haja wala mahitaji

yoyote na manabii na mitume wa Mwenyezi Mungu. Hii ni dalili ya kuondolewa imani. Na yule mtu mwenye fikara kama hii hujidanganya mwenyewe asemapo: Je, kwani mimi sisali, au sifungi, au sitoi shahada? Kwa kuwa yeye hana habari na imani na shauku ya kweli, ndiyo sababu anasema hivi. Yeye anapaswa atafakari kwamba ingawa ni Mungu tu ndiye Amwumbaye mwanadamu, lakini ni kwa namna gani Amemfanya mtu mmoja kuwa sababu ya kuumbwa mtu mwingine. Hivyo, kama vile ndani ya silsila ya kimwili kuna mababa wa kimwili ambao kwao mwanadamu huzalika, halikadhalika ndani ya silsila ya kiroho pia kuna mababa wa kiroho ambao kwao kuzaliwa kwa kiroho hutokea. Zindukeni wala msijidanganye na sura tu ya nje ya Islam na yasomeni kwa kutafakari Neno la Mwenyezi Mungu kwamba ni nini Akitakacho toka kwenu? Yeye Anakutakeni jambo lile lile ambalo kwalo mmefundishwa dua ndani ya sura ya Al Fatiha, yaani dua hii:

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۙ‏ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ[19]

Hivyo, kwa kuwa Mungu Anawasisitizieni kwamba ombeni nyakati tano dua hii kwamba nyinyi pia

[19] *Al-Faatiha*, 1:6-7

mzipate neema zile walizo nazo manabii na mitume, hivyo bila kupitia kwa manabii na mitume mnawezaje kuzipata neema hizo? Hivyo, ililazimika kwamba kila baada ya muda fulani manabii wa Mungu wawe wanakuja kwa ajili ya kukufikisheni kwenye daraja la yakini na upendo ambao kutoka kwao mzipate neema hizo. Je, sasa mtashindana na Mwenyezi Mungu, na kuivunja kanuni yake ya tangu zamani? Je mbegu ya uzazi yaweza kusema kuwa mimi nilikuwa sitaki kuzaliwa kwa njia ya baba? Je masikio yanaweza kusema kuwa sisi hatutaki kusikia kwa njia ya upepo? Hivyo, kunaweza kuwa na ujinga gani zaidi ya huo kwamba ishambuliwe kanuni ya tangu zamani ya Mwenyezi Mungu?

Mwishoni, iwe wazi pia kuwa kuja kwangu katika zama hizi toka kwa Mwenyezi Mungu sio kwa ajili ya kuwarekebisha Waislamu tu, bali lengo ni kuzirekebisha kaumu zote tatu za Waislamu, Wahindu na Wakristo. Na kama vile Mungu Alivyonituma kuwa Masihi Mau'udi kwa Waislamu na Wakristo, vivyo hivyo nilivyo Autaar (Mtume) kwa ajili ya Wahindu. Nami tangu miaka ishirini hivi au zaidi naendelea kutangaza kuwa kwa kuziondolea mbali dhambi zile zilizoijaza dunia, kama vile nilivyo

katika sura ya Masihi mwana wa Mariamu, vivyo hivyo nipo pia katika sura ya Raja Krishana ambaye alikuwa ndiye Autaar mkubwa kuliko Maautaar wote wa dini ya Wahindu, au inapaswa isemwe hivi kuwa kwa sura ya uhakika wa kiroho mimi ndiye yule yule. Haya sio mawazo yangu au makisio yangu, bali Yule Mungu Aliye Mungu wa ardhi na mbingu Ndiye Aliyenidhihirishia haya. Na si mara moja tu bali mara nyingi Aliniambia kwamba ‘U Krishana kwa ajili ya Wahindu, na Masihi Mau‘udi kwa ajili ya Waislamu na Wakristo.’ Nafahamu kuwa Waislamu walio majahili watakaposikia tu habari hii mara moja watasema kuwa kwa kujipa jina la kafiri nimeukubali ukafiri kwa uwazi kabisa. Lakini huu ni wahyi wa Mungu ambao siwezi kukaa bila ya kuudhihirisha, na leo hii ni siku ya kwanza ambapo ninalieleza jambo hili katika mjumuiko mkubwa kama huu, kwa sababu wale watu watokao kwa Mungu huwa hawaogopi lawama ya mlaumu yeyote.

Sasa iwe wazi kwamba, Raja Krishana, kama vile nilivyodhihirishiwa, kwa hakika alikuwa ni mtu aliyekamilika ambaye mfano wake haupatikani kwa Rishi au Autaar yeyote wa Kihindu naye alikuwa ni Autaar, yaani Nabii ambaye Roho mtakatifu alikuwa

akimteremkia toka kwa Mungu. Yeye alikuwa ni mshindi na mwenye ufaulu kutoka kwa Mungu, ambaye aliisafisha ardhi ya nchi ya Maariya (India) kutokana na dhambi. Yeye, kwa hakika alikuwa ni Nabii wa zama zake, ambaye mambo mengi ndani ya mafundisho yake yalipotoshwa huko nyuma. Alikuwa amejaa mapenzi ya Mungu, alikuwa rafiki wa wema na adui wa uovu. Ilikuwa ni ahadi ya Mungu kuwa katika zama za mwisho Amuumbe mfano wake, yaani Autaar. Hivyo, ahadi hii imetimia kwa kudhihiri kwangu. Miongoni mwa funuo zingine zihusikanazo nami ufunuo huu pia ulifunuliwa:

ہے کرشن رُودّر گوپال تیری مہما گیتا میں لکھی گئی ہے

(*Ee Krishna, mwenye kufutilia mbali dhambi, mtunza watu wanyonge, sifa zako zimeandikwa katika Gita*)

Hivyo, mimi nampenda Krishna, mimi ndiye mdhihiriko wake. Na hapa pana siri nyingine katikati kwamba zile sifa anazonasibishwa Krishna (yaani mwangamizaji wa dhambi na mwenye kuwafariji na kuwatunza masikini) sifa hizi hizi ndizo za Masihi Mau'udi. Basi, kana kwamba Krishna na Masihi Mau'udi kiroho ni (mtu) mmoja, tofauti ndiyo tu katika istilahi za kidini. Sasa nikiwa Krishna,

ninawatanababahishia Waaria baadhi ya makosa yao. Moja kati yao ni lile lile ambalo nimelisema pia hapo awali, kwamba njia hii na itikadi hii siyo sahihi kuwa roho na chembechembe zilizoko ulimwenguni ambazo pia huitwa (kwa kihindu) '*Parkurti'* au '*Parmanu'*, havikuumbwa na vilikuwepo tangu azali. Hakuna kisichoumbwa minghairi ya Yule Mungu Ambaye Huishi bila kumtegemea mwingine. Lakini vitu vile vinavyoishi kwa kutegemea wengine haviwezi kuwa vitu visivyoumbwa. Je sifa za roho zipo zenyewe tu na hakuna aliyeziumba? Kama hii ndiyo sahihi, basi roho zaweza pia kuingia zenyewe ndani ya miili, na chembechembe zaweza kukusanyika na kutenganika zenyewe. Kwa njia hii hamtakuwa na dalili yoyote ya kiakili kwa kuamini uwepo wa Mungu. Kwa sababu kama akili inaweza kulikubali jambo hili kwamba roho zote pamoja na sifa zake zote zipatikanazo ndani yake zipo tu zenyewe, basi italikubali kwa furaha sana jambo hili lingine pia kuwa muunganiko au mtenganiko wa roho na miili pia hutokea wenyewe. Na kama njia ya kufanyika kwenyewe ipo wazi, basi hakuna sababu yoyote kwamba njia moja iwekwe wazi na ya pili

ifungwe. Hilo haliwezi kuhakikishwa kwa mantiki yoyote ile.

Halafu kosa hili limewanasisha Waarya ndani ya kosa lingine ambamo mna hasara kwao kama vile ndani ya kosa la kwanza mna hasara kwa Parmeshar (Mungu), nalo ni hili kwamba Waarya wameufanya wokovu kuwa ni wa muda tu, na *Tanasukh* (roho ya mtu kuingia katika mwili mwingine mtu afapo) imefanywa kuwa usumbufu wa kudumu ambao katika huo roho haiwezekani kamwe kujiokoa. Akili timamu haikubali kuunasibisha ubahili na ufinyu huu wa moyo kwa Mungu Aliye Mrehemevu na Mkarimu. Katika hali ambapo Mungu Alikuwa na uwezo wa kutoa wokovu wa milele naye Alikuwa ni mwenye uwezo wote, basi haieleweki kuwa kwa nini Alifanya ubahili wa aina hiyo kwamba Amewanyima waja wake baraka za uwezo wake. Na halafu shutuma hii inazidi kuwa na nguvu ionekanapo kuwa zile roho zilizotiwa ndani ya adhabu kwa muda mrefu na kuandikiwa udhia wa bahati mbaya ya kuzaliwa daima mara kwa mara kwa sura mbalimbali, roho hizo zenyewe hazikuumbwa na Mungu. Jibu lake linalosikika toka kwa Waarya ni hili kwamba Mungu Alikuwa na uwezo wa kutoa wokovu wa milele,

kwani Yu mwenye uwezo wote, lakini wokovu wa muda ulipangwa ili mfufulizo wa *Tanaasukh* usikatike, kwa sababu kuna idadi maalumu ya roho, na haziwezi kuwa zaidi ya hapo, basi kama kungekuwepo na wokovu wa milele, hapo mpango wa kazaliwa kwa sura mbali mbali usingeweza kuendelea. Sababu yake ni kuwa ile roho ambayo baada ya kupata wokovu ikienda penye wokovu itakuwa imeshamponyoka Mungu, na matokeo ya mwisho ya matumizi yale ya kila siku lazima yatakuwa kwamba itafika siku ambapo kutakuwa hakuna hata roho moja itakayobakia mkononi mwa Mungu kuweza kuingizwa katika mpango wa kuzaliwa kwa sura nyingine, na siku fulani shughuli hii ikimalizika basi Mungu Atabakia Akistaafu. Hivyo, kwa sababu ya kulazimika Mungu Akaandaa mpango huu kwamba Akaufanya wokovu uwe wa muda tu. Halafu hapo hapo kukawa na shutuma nyingine kuwa kwa sababu gani Mungu Anawaondoa penye wokovu wale wale wasiokuwa na dhambi ambao walishapata wokovu mara moja na walishatakasika na madhambi? Shutuma hii Mungu Alipangua hivi kwamba yeye Amemuwekea dhambi moja kila mtu Aliyemuingiza mahali pa wokovu na

hatimaye ili kuadhibiwa kwa dhambi hiyo kila roho yatolewa toka katika mahali pa wokovu.

Hizi ndizo kanuni za Waarya. Sasa inpaswa kufanya uadilifu kuwa yule ambaye amenaswa katika shida hizo twawezaje kumwita Mungu. Inasikitisha mno kwamba Waarya, kwa kulikataa jambo la wazi kabisa kwamba Mungu ndiye aliyeumba kila kitu, wamejiingiza ndani ya matatizo makubwa kabisa, na hata kumdhalilisha Mungu kwa kuzikisia kazi Zake kama kazi zao wenyewe, wala hawakufikiria kuwa Mungu katika kila sifa Ametofautiana na viumbe. Na kumpima Mungu kwa vipimo vya sifa za viumbe ni kosa ambalo wataalamu wa mijadala huisema “Kias ma’al farik” (kukisia visivyo). Na kusema kuwa haiwezekani kuwepo kutoka kutokuwepo. Hii ndiyo tajiriba pungufu ya akili kuhusu matendo ya viumbe. Hivyo, kuziingiza sifa za Mungu pia chini ya kanuni hii hii kama sio ukosefu wa fahamu ni nini basi? Mungu Huongea bila ulimi wa kimwili na Husikia bila masikio ya kimwili na Huona bila macho ya kimwili. Halikadhalika Huumba pia bila mahitajio ya kimwili. Kumlazimisha kwa maada ya kuumbia ni sawa sawa na kuzisitisha sifa za Mungu. Halafu ndani ya itikadi hii kuna ufisadi mwingine mkubwa sana

kwamba itikadi hii inaishirikisha kila chembe na Mungu katika sifa ya kuwa tangu azali. Na waabudu masanamu walimshirikisha Mungu na masanamu machache tu, lakini sawa na itikadi hii dunia nzima ni mshiriki wa Mungu, kwa sababu kila chembe inakuwa ni mungu wake binafsi. Mwenyezi Mungu Anajua kuwa mimi siyasemi mambo haya kutokana na bughudha au uadui wowote ule, bali nina yakini kuwa haya kamwe hayakuwa mafundisho ya asili ya 'Veda' (Kitabu kitakatifu cha Wahindu). Nafahamu kuwa hizi ni zile itikadi za wanafalsafa wa kibandia ambao wengi wao hatimaye wakawa Madaharia. Nami nina hofu kuwa kama Waarya hawataachana na itikadi hii basi hatima yao pia itakuwa ni hii hii. Na tawi la itikadi hii ambalo ni *Tanaasukh*, hilo pia linatia doa kubwa kwenye rehema na fadhili ya Mungu, kwani tuonapo kuwa ndani ya sehemu ya shibri mbili au tatu, kwa mfano, siafu wanakuwa wengi kiasi hiki kwamba huwa zaidi ya mabilioni, na ndani ya kila tone la maji mna maelfu ya vijidudu, na mito, bahari na misitu imejaa aina mbalimbali za wanyama na wadudu ambao hatuwezi kulinganisha nao idadi ya binadamu. Katika hali hii wazo linakuja kwamba kama *Tanasukh* ni sahihi basi hadi sasa

Mungu Amefanya nini? Na ni nani Aliyempa wokovu, na itarajiwe nini kwa siku zijazo?

Isitoshe, kanuni hii pia haieleweki kuwa adhabu itolewe lakini mtu anayeadhibiwa asiambiwe kosa lake. Na halafu tena msiba zaidi ni kwamba wokovu hutegemea elimu na elimu inaenda ikitokomea. Na anayezalika kwa sura nyingine yoyote hata kama awe ni Pandit mkubwa namna gani, huwa hakumbuki sehemu yoyote ile ya Veda. Hivyo inafahamika kutokana na hali hii kuwa ni muhali kuupata wokovu kwa kuzaliwa kwa sura nyingine. Na wale wanaume na wanawake wajao duniani kwa mzunguko wa kuzaliwa kwa sura mbalimbali, huwa hawaji na orodha yoyote ya kueleza uhusiano baina yao wa damu ili mtu asipate kumwoa aliyezaliwa upya kwa sura nyingine ambaye kwa hakika ndiye dada yake au mamake!

Na suala la *Neyoga* ambalo siku hizi latumika sana miongoni mwa Waarya, kuhusiana na hilo twasihi mara kwa mara kuwa liachiliwe mbali kadiri iwezekanavyo. Asili ya mwanadamu haitakubali hata kidogo kwamba mtu amruhusu mkewe wa heshima ambaye heshima yake yote inamtegemea yeye, juu ya

yeye kuwa mume wake wa halali, na juu ya kuwepo baina yao uhusiano anaokuwa kati ya mume na mke, halafu kwa tamaa ya kupata watoto amruhusu mkewe mwema kulala na wanaume wengine. Sipendi kuandika zaidi juu ya jambo hili bali naiachia dhamiri ya watu wenye heshima zao. Juu ya hayo yote Waarya wamo katika jitihada ya kuwaita Waislamu kwenye dini yao hii. Basi, tunasema kuwa kila mwenye akili huwa tayari kuukubali ukweli, lakini huu sio ukweli kwamba Mungu Yule Ambaye Amejidhihirisha kwa nguvu Zake kubwa Akataliwe kuwa mwumba na Asiaminiwe kuwa Mdhihiriko wa baraka zote. Mungu wa aina hiyo hawezi asilan kuwa Mungu. Mwanadamu amemtambua Mungu kutokana na nguvu Zake. Wakati ndani mwake nguvu yoyote haikubakia, naye Yu mhitaji kama sisi wa vitu vingine, basi hapo mlango wa Yeye kutambulika utafungwa.

Halafu mbali na hayo, Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kustahili kuabudiwa kwa sababu ya hisani Zake. Lakini kama Yeye Hakuziumba roho wala ndani mwake hamna sifa ya kumfanyia fadhili na hisani mtu pasipo kutenda matendo, sasa mungu kama huyo atastahilije kuabudiwa? Kadiri

tunavyotafakari, tunafahamu kuwa Waarya hawakutoa mfano mzuri wa dini yao. Wakamkubali mungu kuwa dhaifu na mwenye inadi kiasi hiki kwamba akiishatoa adhabu mabilioni bado hatoi wokovu wa milele na hasira yake haipoi abadan. Na Waarya wametia doa jeusi la *Neyoga* kwenye utamaduni wa taifa, na kwa njia hii wameishambulia pia heshima ya wanawake masikini na wametia ufisadi wenye kuaibisha kwenye sehemu zote mbili za haki ya Mungu na haki ya watu. Dini hii inakaribiana sana na Madaharia katika kumstaafisha Mungu, na kutokana na kulingana na *Neyoga* inakaribiana na kaumu isiyostahili hata kutajwa.

Hapa nalazimika kusema kwa uchungu wa moyo kuwa Waarya na Wakristo wengi wamezoea sana kuyashambulia bila sababu mafundisho ya kweli na makamilifu ya Islam, lakini wameghafilika mno kustawisha hali ya kiroho ndani ya dini yao. Dini sio mradi wake kuwa mtu awatukane watu wakubwa na manabii na mitume wote duniani. Kufanya hivi kunapingana na makusudio ya asili ya dini; bali makusudio ya dini ni kwamba mwanadamu baada ya kuitakasa nafsi yake na kila uovu, aifanye roho yake kila wakati iwe imeanguka kwenye kizingiti cha

Mwenyezi Mungu na iwe imejaa yakini, mapenzi, utambuzi, ikhlasi na uaminifu, na ndani yake yapatikane mabadiliko halisi ili kuyapata maisha ya peponi humu humu duniani. Lakini kwa itikadi kama hizo wema wa kweli unaweza kupatikana lini na kwa namna gani ambamo wanadamu wamepewa fundisho hili kuwa mwamini tu damu ya Masihi na halafu mfahamu kuwa mmetakaswa na madhambi. Huu ni utakaso wa aina gani ambao hauhitaji utakaso wowote wa nafsi? Bali utakaso wa kweli hupatikana tu pale mwanadamu anapotubu toka kwenye maisha machafu na kuyatamani maisha yaliyotakasika. Na kwa kuyapata hayo kuna mambo matatu tu yanayohitajika: Kwanza ni mpango na juhudi; yaani kadiri iwezekanavyo ajitahidi kujitoa nje ya maisha maovu. Na ya pili ni dua, yaani kila wakati aendelee kumwomba Mungu ili Amtoe kwa mkono Wake nje ya maisha machafu na Awashe moto ndani yake utakaoziunguza takataka za maovu na kumpatia nguvu itakayozishinda jadhba za nafsi. Na inapaswa adumu hivyo hivyo katika maombi hadi ufike wakati ule ambapo nuru moja ya Mungu ishuke moyoni mwake, na mwonzi ung'aao uangukie nafsi yake ambao uondolee mbali kiza chote na kumwondelea

udhaifu wake na kuzalisha ndani yake mabadiliko matakatifu, kwani bila shaka ndani ya maombi mna athari. Kama wafu wanaweza kufufuka basi ni kwa maombi, na kama wafungwa wanaweza kuachiliwa basi ni kwa maombi, na kama wachafu wanaweza kutakasika basi ni kwa maombi. Lakini kufanya maombi na kufa kuko karibu karibu. Na njia ya tatu ni kuwa pamoja na waliokamilika na walio wema, kwa sababu taa moja yaweza kupata kuwaka kwa njia ya taa nyingine. Ilmuradi, hizi tu ndio njia tatu za kuweza kuepukia madhambi zikiwa pamoja hatimaye fadhili hujaaliwa, na sio kwamba kwa kukubali itikadi ya damu ya Masihi na tujifikirie moyoni mwetu eti sisi tumeokoka na madhambi. Hii ni sawa sawa na kujidanganya wenyewe. Mwanadamu ameumbwa kwa shabaha kubwa, na ukamilifu wake sio tu kwamba aache madhambi. Wako wanyama wengi sana ambao hawafanyi dhambi yoyote ile, je hao wanaweza kusemwa kuwa wamekamilika? Na je sisi kwa njia hii twaweza kupata zawadi toka kwa yeyote yule kuwa sisi hatujakufanyia dhambi yoyote ile? Bali zawadi hupatikana kutokana na huduma za kiuaminifu. Na huduma hiyo ndani ya njia ya Mungu ni hii kwamba mwanadamu awe ni wake tu na

ayavunje mapenzi yote kwa ajili ya mapenzi Yake tu, na aiache ridhaa yake binafsi kwa ajili ya ridhaa Yake. Sehemu hii Kurani Tukufu imetoa mfano mzuri sana nao ni huu kuwa hakuna mwaminio awezaye kukamilika hadi anywe sharubati mbili. Sharubati ya kwanza ni ya kupoza mapenzi ya kutenda dhambi ambayo Kurani Tukufu imeiita jina 'Sharubati ya kafuri': sharubati ya pili ni ya kujaza mapenzi ya Mwenyezi Mungu moyoni ambayo Kurani imeipa jina la sharubati ya *zanjabili* (tangawizi). Lakini inasikitisha kuwa Wakristo na Waarya hawakuishika njia hii. Waarya wameinamia huku kwamba dhambi kwa hali yoyote ile — utubu usitubu — ni yenye kuadhibiwa ambapo mtu atalazimika kuzaliwa duniani mara nyingi isiyohesabika kwa sura mbalimbali tofauti. Na Wakristo nao wanaieleza ile njia ya kuokoka na dhambi ambayo nimeshaieleza sasa hivi. Makundi yote mawili yameshaenda mbali na shabaha hasa, na kwa kuuacha ule mlango uliokuwa wauingie wanatangatanga mbali sana maporini.

Hii nimewaomba Waarya na Wakristo ambao kwa juhudi kubwa wanaieneza dini yao duniani, hali yao ni ya kusikitisha zaidi kuliko Waarya. Waarya siku

hizi wanajaribu kwamba kwa njia yoyote watoke nje kutoka dini yao ya zamani ya kuabudu viumbe, na Wakristo wako katika jitihada sio tu ya kujiingiza wenyewe katika kuabudu viumbe bali na kuiingiza dunia nzima. Kwa kulazimisha tu na kwa kutumia nguvu, Hadhrat Masihi[as] anafanywa kuwa Mungu. Ndani mwake hamjathibitika nguvu yoyote ile makhsus ambayo haipatikani katika manabii wengine, bali baadhi ya manabii walimzidi katika kuonyesha miujiza, na madhaifu yake yanatoa ushuhuda kuwa yeye kwa hakika alikuwa mwanadamu tu. Yeye mwenyewe hakutoa dai lolote lile linalothibitisha kuwa yeye ni mdai wa uungu. Na maneno yake yote yale ambayo kwayo uungu wake unafahamika, kufahamu namna hiyo ni makosa. Maelfu ya maneno ya aina hiyo hutokea kwa manabii wa Mungu kwa njia ya istiara na majazi, kutoa humo madai ya uungu sio kazi ya mwenye akili bali ni kazi ya wale tu ambao huwa na shauku tu ya kumfanya mwanadamu kuwa Mungu. Nami naweza kusema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa ndani ya wahyi na ufunuo wangu mna maneno zaidi ya hayo. Hivyo, ikiwa kutokana na maneno hayo uungu wa Hadhrat Masihi[as] unathibitika, basi hata mimi (Mungu Apishe mbali)

ninakuwa na haki ya kutoa pia madai haya haya. Hivyo, kumbukeni kuwa madai ya uungu juu ya Hadhrat Masihi[as] ni tuhuma tu moja kwa moja. Yeye kamwe hakutoa madai ya aina hiyo. Chochote alichokisema kuhusiana na yeye binafsi, neno hilo halikiuki mpaka wa uombezi. Hivyo nani aukataaye uombezi wa manabii? Kwa uombezi wa nabii Musa[as] mara nyingi sana wana wa Israeli waliokolewa na adhabu iwakayo. Na mimi binafsi ninao uzoefu huo. Na waheshimiwa wengi wa Jumuiya yangu wanafahamu vema kuwa kutokana na uombezi wangu baadhi ya waliokumbwa na misiba na maradhi waliondolewa maumivu yao, nao walikuwa wakipewa habari hizi mapema. Na kusulubiwa kwa Masihi kwa ajili ya kuokolewa umati wake na kumtupia madhambi ya umati wake ni itikadi isiyo na maana ambayo iko mbali sana na akili. Ni mbali sana kutoka kwa sifa ya Mungu ya uadilifu kwamba mtu fulani afanye dhambi halafu adhabu apewe mwingine. Ilmuradi itikadi hii ni mjumuiko wa makosa. Kumuacha Mungu Mmoja Asiye na mshirika na kuwaabudu viumbe sio kazi ya wenye akili. Na kusema zipo nafsi tatu zijitegemeazo na zilizo kamilifu ambazo zote ni sawa sawa katika ujalali na

nguvu, na halafu hizo zote tatu kuzifanya kuwa ni mungu mmoja aliyekamilika, hiyo ni mantiki ambayo inahusikana na Wakristo tu duniani. Halafu sehemu ya kuhuzunisha ni kwamba yale makusudio ambayo kwayo mpango huu mpya ulipangwa, yaani kuokoka na dhambi na kuepukana na maisha machafu ya kidunia, makusudio hayo pia hayakupatikani. Bali kama vile hali ya wanafunzi wa Yesu ilivyokuwa safi kabala ya kafara nao hawakuijali dunia wala pesa za dunia na hawakuwa wamenasa ndani ya uchafu wa dunia, na juhudi yao haikuwa kwa ajili ya kuchuma dunia, wapi ulibakia moyo wa aina hii kwa watu wa baadaye baada ya kafara? Hasa katika zama hizi kadiri kafara na damu ya Yesu zinavyotiliwa mkazo ndivyo wanavyozidi Wakristo kunasa katika dunia na wengi wao kama mlevi wanajishughulisha kutwa kucha katika mambo ya kidunia. Na hapa hakuna haja ya kutaja madhambi mengine yanayoenea Ulaya, hasa ulevi na uzinzi.

Sasa nitamalizia hotuba yangu kwa kuwaeleza wasikilizaji kwa jumla baadhi ya uthibitisho wa madai yangu. Enyi wasikilizaji waheshimiwa, Mwenyezi Mungu Avifungue vifua vyenu kwa ajili ya kupokea haki na Akufunulieni ufunuo wa

kuifahamu haki. Mtakuwa mnalifahamu jambo hili kuwa kila Nabii na Mtume na Mjumbe wa Mungu ambaye huja kwa ajili ya kuwarekebisha watu, ingawa kwa ajili ya kumtii yeye yatosha kiakili kuwa chochote asemacho ni kweli tupu, ndani yake hamna uongo wowote au udanganyifu, maana akili timamu haihitaji mwujiza wowote katika kuukubali ukweli, lakini kwa kuwa ndani ya asili ya mwanadamu mna nguvu pia ya kushuku kwamba ingawa jambo hili kwa hakika ni sahihi, la ukweli na haki, lakini hata hivyo mwanadamu bado anashuku kwamba isije kukawa na kusudio fulani makhsus kwa huyo anayeeleza au isiwe amedanganyika au amedanganya. Na wakati mwingine kwa sababu ya kuwa kwake mtu wa kawaida neno lake halitiliwi maanani na hufahamika kuwa ni hakiri na dhalili. Na wakati mwingine tamaa za nafsi inayoshawishi kwenye maovu huwa zinashamiri kiasi hiki kwamba hata kama ieleweke kuwa yote yaliyosemwa ni kweli hata hivyo nafsi inakuwa imeelemewa na jadhba zake chafu kiasi ya kwamba anakuwa hawezi kutembea juu ya njia hii ambayo mtoa mawaidha na nasaha anataka kumtembeza, au udhaifu wa asili unamzuia asinyanyue hatua. Hivyo, hekima ya Mungu imetaka

kwamba wale watu wanaokuja makhsus kutoka kwake wawe pia na ishara kadha za msaada wa Mungu ambazo pengine zadhihirika kwa sura ya rehema na pengine kwa kura ya adhabu, na watu hao kutokana na ishara hizo huitwa kuwa watoao habari njema na waonyaji toka kwa Mungu. Lakini wale waaminio hupata sehemu ya ishara za rehema ambao hawafanyi kiburi mbele ya amri za Mungu na hawawahakirishi wala hawawadhalilishi waliotumwa na Mungu, na kwa busara zao walizopewa na Mungu huwatambua watu hao, na wakishikilia kwa nguvu njia ya ucha Mungu huwa hawakithiri katika ubishi, na wala hawajitengi kutokana na kiburi cha kidunia na heshima za kibandia, bali waonapo kuwa mtu mmoja amesimama katika wakati muafaka sawa na suna ya manabii, aitaye kwa Mwenyezi Mungu, na maneno yake ndiyo ambayo kuyakubali kuwa sahihi ipo njia moja na ndani yake mnapatikana ishara za msaada wa Mungu, ucha Mungu na uaminifu, na sawa na kipimo cha suna za Manabii hakuna shutuma yoyote ipatikanayo katika kauli yake na vitendo vyake, basi humkubali mtu kama huyo. Bali wapo pia baadhi ya wenye bahati ambao kwa kuona sura tu wanafahamu kuwa hii sio sura ya mwongo na

mdanganyifu. Basi ishara hudhihirika kwa ajili ya watu wa aina hiyo. Nao kila wakati kwa kupata nguvu ya imani kutokana na kukaa pamoja na mkweli na kushuhudia mabadiliko matakatifu huendelea kuziona ishara mpya mpya na kweli zote na maarifa na nusura zote na misaada yote na kujulishwa mambo ya ghaibu ya kila aina huwa ishara tu kwao, nao kutokana na fahamu nyepesi wakiihisi hata misaada myepesi sana ya Mwenyezi Mungu kwa huyo mjumbe wanapata pia habari za ishara nyepesi kabisa. Lakini kinyume nao wako pia wale watu ambao hawanayo sehemu ya ishara za rehema, kama vile kaumu ya Nuhu hawakupata mwujiza wa aina yoyote isipokuwa mwujiza wa kugharikisha, na kaumu ya Luti haikufaidika na mwijiza wowote isipokuwa mwujizia huu kuwa ardhi yao ilipinduliwa juu chini nao wakavurumishiwa mawe. Halikadhalika katika zama hizi Mungu Amenituma. Mimi naona kuwa tabia za watu wengi wa zama hizi zinafanana na tabia za kaumu ya Nuhu. Miaka mingi imepita ambapo ishara mbili zilidhihirika mbinguni kwa ajili yangu, na hiyo ilikuwa bishara iliyosimuliwa na ukoo wa Nabii s.a.w. nayo ni hii kwamba wakati Imamu wa zama za mwisho atakapodhihiri duniani basi kwa ajili yake

zitadhihirika ishara mbili ambazo hazijawahi kudhihirika kwa ajili ya yeyote mwingine. Yaani ni hivi kwamba mnamo mwezi wa Ramadhani mwezi utapatwa mbinguni, na kupatwa huko kutatokea ndani ya usiku wa kwanza wa mausiku ya kawaida ya kupatwa mwezi, na siku hizo hizo ndani ya Ramadhani hiyo hiyo jua pia litapatwa, na kupatwa huko kutakuwa katika siku ya katikati ya siku za kawaida za kupatwa kwa jua. Na bishara hiyo ilikubaliwa na Masunni na Mashia, na iliandikwa kwamba tangu kuumbwa kwa dunia haijawahi kutokea kwamba mwenye kudai uimamu alikwepo na katika zama zake matukio yote haya mawili yakadhihiri katika tarehe hizo hizo. Lakini itatokea hivyo katika zama za Imamu wa zama za mwisho, na ishara hiyo itakuwa makhsus kwa ajili yake. Na bishara hiyo ilikuwa imeandikwa ndani ya vitabu vilivyoenea duniani tangu miaka elfu iliyopita. Lakini bishara hii ilipotimia katika zama za mimi kudai kuwa Imamu, basi hakuna yeyote aliyeikubali, na hakuna hata mtu mmoja aliyeiona bishara hii adhimu na kufanya baiati yangu, bali wakazidi kutoa matusi na kufanya dhihaka. Wakaniita dajjali, Kafiri, mwongo na kadha wa kadha. Hii ilitokea hivi kwa

kuwa bishara hii haikuwa kama adhabu, bali rehema ya Mungu ilitoa ishara kabla ya kutokea kwake, lakini watu hawakufaidika kitu kutokana na ishara hii, wala mioyo yao haikuelekea kwangu hata kidogo, kana kwamba hiyo haikuwa ni ishara, ilikuwa ni bishara ya kipuuzi tu iliyotolewa. Halafu baada yake, wakati kelele za wapingaji zilipovuka mipaka, basi Mungu Akaonyesha ishara ya adhabu ardhini, kama vile tangu azali ilivyoandikwa ndani ya vitabu vya Manabii. Na ishara hiyo ya adhabu ni tauni ambayo inaitafuna nchi hii tangu miaka michache iliyopita na hakuna mpango wowote wa kibinadamu uwezao kufaa chochote mbele yake. Habari ya tauni hii imo kwa maneno ya wazi kabisa ndani ya Kurani Tukufu, kama vile Mwenyezi Mungu Asemavyo:

وَاِنۡ مِّنۡ قَرۡيَةٍ اِلَّا نَحۡنُ مُهۡلِكُوۡهَا قَبۡلَ يَوۡمِ الۡقِيٰمَةِ اَوۡ مُعَذِّبُوۡهَا عَذَابًا شَدِيۡدًا ؕ[20]

Yaani, muda kidogo kabla ya Kiama tauni kali sana itashambulia na kwayo baadhi ya vijiji vitaangamia kabisa na baadhi yao vitapata adhabu kiasi fulani na kusalimika. Na vivyo hivyo katika aya nyingine Mwenyezi Mungu Anasema ambayo tafsiri yake ni

---

[20] Na hakutakuwa mji ila Sisi Tutauhilikisha kabla ya siku ya Kiyama au kuadhibu adhabu kali. *Banii Israaiil*, 17:59

hii kwamba itakapokaribia Kiama, Tutamtoa mdudu fulani toka ardhini atakayewang'ata wanadamu kwa sababu hawakuzikubali ishara zetu. Aya zote hizi mbili zimo ndani ya Kurani Tukufu, nayo ni bishara ya wazi kabisa ihusikanayo na tauni, kwa sababu tauni pia ni aina fulani ya mdudu ingawa matabibu wa zamani hawakuwa na habari juu ya mdudu huyu. Lakini Mwenyezi Mungu Aliye na elimu ya ghaibu Alikuwa Anafahamu kuwa mzizi wa tauni kwa asili ni mdudu fulani atokaye ardhini ndio sababu Akampa jina la "*Daabbatul Ardh*", yaani mdudu wa ardhini. Ilmuradi, ishara ya adhabu ilipodhihiri na maelfu ya watu wakafa ndani ya Panjab, na nchi hii ilitetemeka, hapo baadhi ya watu wakazinduka na ndani ya muda mfupi watu karibu laki mbili wakafanya baiati na hadi sasa baiati zinaendelea kufanywa kwa wingi, kwa sababu hadi sasa tauni bado haijaacha mashambulizi yake. Na kwa sababu hiyo imekuja kama ishara, kwa hiyo maadamu watu wengi hawatakuwa wamefanya mabadiliko ndani yao, basi hakutakuwa na matumaini kuwa maradhi haya yanaweza kuondoka nchini. Ilmuradi nchi hii inafanana sana na nchi ya zama za Nuhu kwamba kwa kuona ishara ya kimbingu hakuna yeyote aliyeamini, na kwa kuona ishara ya adhabu

maelfu ya watu wamefanya baiati. Na manabii waliopita waliitaja ishara hii ya tauni. Hata ndani ya Injili imetajwa kuwa tauni itashambulia katika wakati wa Masihi Mau‘udi na vita pia vimetajwa ambavyo vinaendelea hivi sasa.

Hivyo, enyi Waislamu! tubuni, nyinyi mwaona kuwa kila mwaka tauni hii inakutenganisheni na wapenzi wenu. Elekeeni kwa Mungu ili Naye Akuelekeeni. Na kwa sasa haifahamiki kuwa muda wa tauni ni hadi lini na nini kitakachotokea. Ikiwa mna shaka kuhusiana na madai yangu na utafutaji wa ukweli pia upo, basi ni rahisi sana kuiondoa shaka hiyo, kwa sababu ukweli wa kila nabii hutambulika kwa njia tatu:

Kwanza, kwa akili. Yaani yapasa kutazama kwamba wakati aliojia nabii au mtume huyo akili inatoa ushahidi au la kwamba wakati huo kulikuwa na haja ya ujio wake au la? Na hali ya wanadamu ilikuwa inahitaji au la kwamba kwa wakati huo aje mrekebishaji yeyote?

Pili ni bishara za Manabii waliopita. Yaani inafaa kutazama kuwa kuna Nabii yeyote hapo kabla aliyewahi kutoa bishara juu yake au juu ya zama zake ya kudhihiri kwa yeyote au la?

Tatu ni nusura ya Mungu na msaada wa kimbingu. Yaani, inafaa kutazama kwamba je pamoja naye kuna msaada wowote wa kimbingu au la?

Hizi alama tatu zimewekwa tangu zamani kwa kumtambua mkweli aliyetoka kwa Mungu. Sasa, enyi marafiki! Mungu Akiwarehemuni Amezijumuisha sehemu moja alama zote hizi tatu kwa kunisadikisha. Sasa mkipenda kubalini au msikubali. Ikiwa mtazame kwa mtazamo wa kiakili, basi akili timamu inalalamika na kulia kwamba kwa wakati huu Waislamu wanahitaji mrekebishaji mmoja toka mbinguni. Hali zao za ndani na nje zinatisha, na Waislamu kana kwamba wamesimama karibu na shimo, au wamesibiwa na mafuriko makali. Ikiwa mtatafuta ndani ya bishara za zamani, basi nabii Danieli pia alitoa bishara kunihusu na kuhusu zama zangu hizi, na Mtume Mtukufu[saw] pia alisema kuwa Masihi Mau'udi atazaliwa katika umati huu huu. Kama kuna yeyote ambaye hafahamu, basi na atazame *"Sahihi Bukhari"* na *"Sahihi Muslim"*, na aisome pia bishara ya ujaji wa Mujaddidi mwanzoni mwa karne. Na kama atake kuitafuta nusura ya Mungu kuhusiana nami, basi ikumbukwe kuwa hadi sasa ishara elfu zimeshadhihirika.

Miongoni mwao ni ishara ile ambayo iliandikwa miaka ishirini na minne iliyopita ndani ya *"Barahine Ahmadiyya"* na iliandikwa wakati ambapo sikuwa hata na mtu mmoja aliyefanya baiat yangu wala hakukuwa na yeyote aliyefunga safari kunijia. Na ishara hiyo ni hii kwamba Mwenyezi Mungu Anasema:

ياتيك من كلّ فجّ عميق- ياتون من كلِّ فجّ عميق-

yaani, unakuja wakati ambapo misaada ya mali itakufikia toka kila upande na maelfu ya watu watakujia. Na halafu Anasema:

ولا تصعر لخلق اللّٰه و لا تسئم من الناس

Yaani, watu watakuja wengi kiasi hiki kwamba utashangazwa na wingi wao. Basi, inatakiwa usiwatendee kwa khulka mbaya na wala usichoke kukutana nao.

Hivyo, enyi wapenzi! Ingawa hamna habari hii kwamba ni watu kiasi gani wamenijia Qadian na kwa uwazi kiasi gani bishara hiyo imetimia, lakini katika mji huu huu mtakuwa mmeshuhudia kuwa maelfu ya watu wa mji huu huu walijumuika stesheni kwa ujio

wangu kwa kuniona, na mamia ya wanaume kwa wanawake wa mji huu wamefanya baiati, nami ndimi yule yule mtu ambaye tangu miaka saba au minane kabla ya zama za *"Barahine Ahmadiyya"* nilishaishi katika mji huu huu kwa karibu miaka saba na hakukuwa na yeyote aliyekuwa anahusiana nami wala hakukuwa na yeyote aliyekuwa akiijua hali yangu. Basi, sasa mfikiri na kuzingatia kwamba miaka ishirini na minne kabla ya umaarufu huu na watu wengi kunijia, ilitolewa katika kitabu changu '*Barahine Ahmadiyya*' bishara hii kuhusiana nami katika wakati ambao sikuwa kitu machoni mwa watu. Ingawa, kama nilivyokwisha eleza, katika siku za karibu za uandishi wa kitabu cha *"Barahine Ahmadiyya"* nilishaishi takriban miaka saba ndani ya mji huu huu, hata hivyo miongoni mwenu watakuwemo watu wachache wanaonifahamu, kwa sababu katika zama hizo mimi nilikuwa ni mtu asiyejulikana na nilikuwa mtu wa kawaida nami katika mtazamo wa watu sikuwa na taadhima wala heshima yoyote. Lakini zama hizo zilikuwa nzuri sana kwa ajili yangu kwamba katika makusanyiko ulikuwa upweke na katika wingi ulikuwepo umoja, nami nikaishi mjini kama mtu aliye msituni. Mimi

naupenda mji huu kama niipendavyo Qadian, kwa sababu sehemu moja ya umri wangu wa awali nimepitisha humu na nimeshazunguka mara nyingi ndani ya mitaa ya mji huu. Rafiki yangu mwaminifu wa zama hizo katika mji huu ni mzee mmoja, yaani bwana Hakim Husamuddin ambaye wakati huo pia alikuwa ananipenda sana, yeye anaweza kutoa ushahidi kwamba hizo zilikuwa ni zama za aina gani na jinsi nilivyokuwa sijulikani kabisa. Sasa mimi nawaulizeni nyiye kwamba katika zama kama hizo kutoa bishara yenye shani kubwa kwamba mtu asiyejulikana kiasi hiki hatimaye atakuja kunyanyuka kiasi hiki kwamba malaki ya watu watakuja kuwa wafuasi wake na makundi kwa makundi watu watafanya baiati yake, na juu ya upinzani mkali wa maadui mwelekeo wa watu kunijia hautaathirika, bali watu watakuwa wengi sana hata kukaribia kukuchosha, je hii imo ndani ya uwezo wa mwanadamu? Na je, kuna mzushi yeyote awezaye kutoa bishara kama hii kwamba miaka ishirini na minne kabla, katika zama za upweke na unyonge, atoe habari za mnyanyuko huu na mwelekeo huu wa watu kumjia? Kitabu cha *"Barahine Ahmadiyya"* ambamo bishara hii inapatikana si kitabu

kisichojulikana, bali katika nchi hii kipo kwa Waislamu, Wakristo na Waarya na hata kipo serikalini. Ikiwa yeyote aitilie shaka ishara hii kubwa basi anatakiwa aonyeshe mfano wake duniani. Na mbali na hiyo kuna ishara zingine nyingi zinazofahamika katika nchi hii. Baadhi ya wajinga ambao hawaridhii kuukubali ukweli, wao hawafaidiki chochote na ishara hizo zilizothibitika, nao hutafuta njia ya kukengeuka kwa kutoa lawama za ovyo, na kwa kuitolea lawama bishara moja au mbili wanayatilia vumbi maelfu ya bishara na ishara nyingine. Yasikitisha kwamba waongopao hawamwogopi Mungu hata kidogo, na watungapo uzushi hawakumbuki mkamato wa Akhera. Mimi sina haja ya kuueleza kwa kirefu uzushi wao na kuwasikilizisha wasikilizaji hali zao zote. Kama kungekuwa na ucha Mungu ndani yao, kama ndani mwao mngekuwa na hata chembe ya hofu ya Mungu, wasingefanya haraka kuzikadhibisha ishara za Mwenyezi Mungu. Na kama tuseme kwamba hawakuifahamu ishara fulani basi walitakiwa kuniuliza uhakika wake kiubinadamu na kwa upole. Shutuma kubwa mojawapo ni hii kwamba Atham hakufa katika muda uliowekwa, na ingawa Ahmad

Beg alikufa kama vile bishara ilivyosema, lakini mkwe wake ambaye alijumuishwa ndani ya bishara hii hakufa. Huu ndio ucha Mungu wa watu hawa kwamba hawaongelei hata kidogo maelfu ya ishara zilizokwisha timia, na mara kwa mara wanaitaja bishara moja au mbili ambazo hawakuzielewa na kuzipigia kelele katika kila mjumuiko. Kama kungekuwa na hofu ya Mungu basi wangefaidika na ishara na bishara zile zilizokwishathibitika. Hii sio njia ya watu wakweli kwamba waikengeuke miujiza ya wazi wazi, na kama liwepo jambo gumu la kueleweka, basi hapo walitolee lawama. Kwa njia hii mlango wa kuwaletea lawama manabii wote utafunguka, na hatimaye watu wenye mwenendo wa aina hii watajitenga na wote. Kwa mfano, kuna shaka gani kuhusu miujiza ya Hadhrat Isa[as]. Lakini mpinzani mwenye shari anaweza kusema kuwa baadhi ya bishara zake zilithibitika kuwa ni za uongo kama vile hadi sasa Wayahudi wanasema kwamba hakuna bishara yoyote ya Masihi Yesu iliyotimia. Alisema kwamba ‘wanafunzi wangu kumi na wawili wataketi peponi juu ya viti kumi na viwili’. Lakini wale kumi na wawili wakabakia kumi na mmoja, na mmoja akaritadi. Halikadhalika alisema kwamba

watu wa zama hizi hawatakufa hadi nitakaporudi, ilhali achilia mbali zama hizo, watu wa karne kumi na nane wameshaingia makaburini naye hadi sasa hajaja na bishara yake ilithibitika kuwa ni ya uongo katika zama hizo hizo. Na alisema kuwa mimi ni mfalme wa Wayahudi, lakini hakuupata ufalme wowote. Kuna shutuma nyingi nyingine za aina hii. Vivyo hivyo katika zama hizi baadhi ya watu wenye tabia chafu wakitoa shutuma dhidi ya baadhi ya bishara za Mtume[saw] na kuzikataa bishara zake zote. Na baadhi yao hutoa kisa cha Hudaibiya. Sasa kama shutuma hizo zastahili kukubalika, basi mimi niwasikitikie nini watu hao. Lakini kuna hofu hii kwamba kwa kuifuata njia hii isije hata wakaiaga Islam. Ndani ya bishara za Manabii wote, halikadhalika ndani ya bishara zangu, mmeingia pia *ijtihadi* (kufumbua maana ya bishara), kama vile katika safari ya Mtume[saw] ya kwenda Hudaibiya pia *ijtihadi* iliingia ndipo alipofunga safari. Lakini *ijtihadi* hiyo haikutokea kuwa sahihi. Hakuna tofauti yoyote ipatikanayo katika shani, ujalali na hadhi ya nabii kwa kosa kupatikana katika *ijtihadi* yake. Ikiwa mseme kuwa itibari itatoweka kutokana na hali hiyo, basi jibu lake ni hili kuwa upande wa wingi unailinda itibari hiyo. Wakati mwingine Wahyi

wa Nabii unakuwa kama *khabari wahid* (yaani unatakiwa kufikiriwa sana ili kuizingatia muradi wake hasa) pamwe na ufupisho. Na wakati mwingine Wahyi kuhusu jambo fulani unakuwa kwa wingi na kwa uwazi. Hivyo, kama kuhusu wahyi ule kwa sura ya ufupisho litokee kosa lolote wakati wa kuufafanua, basi bishara zilizo wazi na imara hazitapata dhara yoyote kwa sababu hiyo. Basi mimi siwezi kulikataa kwamba wakati mwingine hata wahyi wangu pia uwe kama *khabari wahid* na uwa kwa ufupisho na litokee kosa wakati wa kuufafanua, Manabii wote wanashiriki katika jambo hili; laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya waongo. Isitoshe, kuhusiana na matabiri ya maonyo Mungu Halazimiki kuyatimiza. Utabiri wa nabii Yunus ni shahidi juu ya jambo hili. Na manabii wote wanaafikiana juu ya jambo hili kwamba nia za Mungu zinazokuwa kuonya zaweza kutanguka kwa sadaka na maombi. Hivyo, kama utabiri wa maonyo hauwezi kutanguka, basi sadaka na dua hazina maana.

Sasa naimaliza hotuba hii na kumshukuru Mwenyezi Mungu Ambaye Amenipa uwezo wa kuiandika juu ya mimi kuumwa na kudhoofika kimwili. Nami naomba dua kwa Mungu kwamba Aifanye hotuba hii iwe

sababu ya mwongozo kwa wengi. Na kama vile katika makutano hayo inavyonekana mjumuiko wa kidhahiri, vivyo hivyo ndani ya mioyo yote Atie ushirikiano na upendo kuhusiana na mwongozo, na kila upande Apeperushe mwongozo. Macho hayawezi kuona chochote bila ya nuru ya mbinguni, hivyo Mungu Ateremshe nuru ya kiroho toka mbinguni ili macho yaweze kuona, na aumbe hewa toka kwa ghaibu ili masikio yasikie. Nani awezaye kuja upande wangu ila yule tu ambaye Mungu Amvute kwangu. Wengi Anawavuta na Atawavuta. Na Atazivunja kufuli nyingi. Mzizi wa madai yangu ni kifo cha Hadhrat Isa[as]. Mungu Huumwagilia maji mzizi huu kwa mkono Wake na Mtume anaulinda. Mungu kwa kauli, na Mtume Wake kwa kitendo, yaani kwa kujionea kwa macho amelitoa ushahidi kuwa Hadhrat Isa[as] amekufa, na katika usiku wa Mi‘raji alimuona Hadhrat Isa[as] miongoni mwa roho za wafu. Lakini yasikitisha kuwa hata hivyo watu bado wanamfahamu kuwa yu hai, na wanampa sifa ambayo hakupewa nabii mwingine yeyote. Ni mambo haya haya ambayo kwayo dhana ya Wakristo ya uungu wa Yesu hupata nguvu, na watu wengi wasio imara hudanganyika na

itikadi za aina hii. Mimi ni shahidi kwamba Mungu Amenipasha habari kuwa Hadhrat Isa[as] ameshafariki. Kumfanya sasa kuwa hai ni maangamio ya dini. Na kung'ang'ania tu katika mawazo haya ni kuchekecha tu vumbi bila sababu. Ijmaa (rai muafaka ya waaminio) ya kwanza ndani ya Islam ilikuwa ni hii hii kwamba hakuna nabii yeyote miongoni mwa manabii waliopita aliye hai kama vile inavyothibitisha aya:

مَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ؕ[21]

Mungu Ampe ujira mwingi sana Abu Bakar[ra] ambaye ndiye alikuwa sababu ya Ijmaa hii; akawasomea aya hii akipanda juu ya mimbari.

Mwishoni twaishukuru serikali ya Kiingereza kwa moyo wa kweli kabisa ambayo kutokana na ukunjufu wa moyo wake imetupatia uhuru wa kidini. Uhuru huu ambao kwa sababu yake tunawafikishia watu elimu ya muhimu mno ya kidini, hii sio neema ile ambayo kwayo tuitolee tu shukrani ya kawaida serikali hii, bali yastahili kushukuru kwa dhati ya

---

[21] Na siye Muhammad ila yu Mtume. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume. *Aali 'Imraan*, 3:145

moyo. Kama serikali hii adhimu ingetupatia ardhi ya malaki, lakini isingetupatia uhuru huu, basi twasema kwa ukweli kabisa kuwa ardhi hiyo isingekuwa sawasawa na uhuru huu, kwa sababu mali ya dunia ni yenye kuangamia, lakini hii ni mali isiyoangamia. Nainasihi Jumuiya yangu kuwa wawe na shukrani ya dhati kwa serikali yetu hii yenye hisani, maana yule asiyemshukuru mwanadamu, huwa hamshukuru Mungu pia. Mtu mwema ni yule tu ambaye kama vile amshukuruvyo Mwenyezi Mungu amshukuru yule mwanadamu pia ambaye kwaye neema yoyote ilimfikia toka kwa Mtoa neema wa kweli. Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo.

**Mwandishi: Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian**
1 Novemba 1904, siku ya Jumanne,
Sialkot

**(Shairi la Kiajemi)**

*Amri ya mbingu naifikishia ardhi, kama niisikie na nisiwafikishie watu, basi niende nayo wapi?*

*Mimi nimetumwa tu, sina hiari katika kazi hii; nenda, mkaulize jambo hili Mungu Aliyenituma.*

*Ni masikitiko kwamba niwapendao hawaku nitambua; Watanitambua nitakapoaga dunia hii!*

*Kila usiku napata huzuni elfu nikiumia kwa kuona hali mbaya ya kaumu. Ee Mola! Uniokoe na zama hizi za machafuko.*

*Mbali na njia yangu, njia yoyote watakaoipenda si chochote. Yu mwenye bahati mbaya ambaye machoni mwake kilicho duni ni chenye heshima.*

*Baada ya Mungu nimelewa kwa mapenzi ya Muhammad; kama hii ni kufuru, basi Wallahi mimi ndiye kafiri mkubwa sana.*

*Roho yangu yayeyuka kwa kuhuzunikia imani yako, Ee mpendwa; lakini ni la ajabu kwamba katika dhana yako mimi ni kafiri.*

*Ee Mola, kwa machozi yangu Uuoshelee mbali uzembe wao, kwani kwa huzuni hii leo hata malalo yangu yamepata kuloa.*

*Najitolea uhai wangu kwa dini ya Mustafaa*[saw]*, huu ndio utashi wa moyo wangu, laiti upate kutimia.*

✵✵✵